BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,010,689,585/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 5

**SERIKALI** yamwaga ajira 1,600, nafasi 16 zakosa waombaji



ARSENAL KUMREJESHA GNABRY

UKURASA 22


# Nipashe

Jumamosi Julai 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580994

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Utata kufutwa ada kidato cha 5 na 6



**Shule** hazina mwongozo, wazazi wailipa, serikali yaandaa tamko... *Uk. 2*

UKURASA WA 3

## MFANYAKAZI WA TANESCO AFARIKI DUNIA AKIWA 'GESTI'

MFANYAKAZI wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Katavi, amekutwa amefariki katika nyumba ya kulala wageni iliyoko Manispaa ya Mpanda mkoani humo...

UKURASA WA 4

## WAHOFIWA KUFA MAJI WAKIVUSHA NG'OMBE

WATU watatu wanadaiwa kufariki dunia baada ya kuzama maji kwenye Mto Rufiji wakati wakijaribu kuvusha ng'ombe wa mfugaji kutoka Kitongoji cha Shaurimoyo, Kijiji cha Nyamwage, Rufiji mkoani Pwani kuelekea Kijiji cha Mtanange ...

UKURASA WA 5

## MKURUGENZI AINGIA MATATANI KUKACHA ZIARA YA MKUU MKOA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, amepiga marufuku Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa zilizopo mkoani humo kutuma wawakilishi wao kama hakuna ulazima anapofanya ziara zake za kusikiliza kero za wananchi...



Upasuaji wa kuwatenganisha watoto waliokuwa wameungana Neema na Rehema, ukifanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam jana, ambapo umekuwa na mafanikio chini ya jopo la wataalamu 31 waliotumia saa saba kuukamilisha. **PICHA: MNH**

## Utenganishaji watoto pacha wafanikiwa

UKURASA 2

# Madiwani 9, kigogo wa CCM kortini shtaka mauaji Loliondo

UK. 2

**MICHEZO** YANGA, COASTAL KAZI MOJA TU LEO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Utata kufutwa ada kidato cha 5 na 6

**Na Waandishi Wetu**

UTATA umeibuka kuhusu kufutwa kwa ada ya shule kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita nchini, wazazi wakilipa ada hiyo kwa mwaka huu wa masomo huku serikali ikisema itatoa tamko ikiwa watarejeshewa fedha au la.

Akiwasilisha bungeni mwezi uliopita mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipendekeza kufuta ada kwa kidato cha tano na cha sita ili kuwapunguzia gharama wanafunzi.

Hatua hiyo ina maana kwamba ada sasa haitakuwapo kwa shule za serikali kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita baada ya serikali kuanza kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo, maarufu Elimu Bure, mwaka 2016.

Waziri Nchemba alibainisha kuwa kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni 90,825 na kidato cha sita ni 56,880 na mahitaji ya fedha ni Sh. bilioni 10.339.

"Kwa hatua hii, elimu bila ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita. Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati kadri hali ya uchumi itakavyotengemaa," Dk. Mwigulu alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa serikali imeendelea kugharamia programu ya elimumsingi bila ada ambapo hadi Aprili mwaka huu, Sh. bilioni 244.5 zilitolewa.

Licha ya Bunge kuridhia mapendekezo hayo, Nipashe imebaini katika shule kadhaa ilizofuatilia utekelezaji wa uamuzi huo, zikiwamo za Mara, Dodoma, Dar es Salaam na Kilimanjaro, ada hiyo imelipwa na wazazi wa wanafunzi waliojiounga na kidato cha tano mwaka huu, pia walioingia kidato cha sita kwenye shule zinazomilikiwa na serikali.

**KAULI YA SERIKALI**

Alipoulizwa na Nipashe jana kuhusu utata huo wa ada ya kidato cha tano na sita kulipwa licha ya serikali kutoa tamko la kuifuta, Kamishna wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema suala hilo watalitolea tamko baadaye.

"Mwanafunzi yeye akae aendelee na shule, hilo suala tutatoa tamko baadaye. Tunataka tukae tuone tamko la kufutwa ada utekelezaji wake unaanza lini na kuamua waliolipa kama wanapaswa kurejeshewa ili ziandikwe barua.

"Kwa hiyo, inahitaji kukaa kuamua hilo jambo litekelezwe vipi, tutasema baadaye," Dk. Lyabwene alisema katika ufafanuzi wake kwa Nipashe.

Wakati wa kuahirisha mkutano wa Bunge juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, pamoja na mambo mengine, alitoa ufafanuzi kuhusu ugharamiaji wa elimu unavyotekelezwa na serikali kupitia Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo.

Alisema kuwa serikali kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015 na Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015, umetoa maelekezo bayana kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila ada.

Waziri Mkuu alisema maekezo hayo ni pamoja na matumizi ya fedha za utawala ambazo hutolewa Hazina na kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za shule za msingi na sekondari nchini kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati, uendeshaji wa mitihani ya ndani na utawala.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Jumanne Muliro (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kufungua kikao cha mtandao wa Polisi wanawake (TPFNET), jijini humo jana. Kushoto ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa kipolisi Ilala ACP, Debora Magiligimba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madiwani 9, kigogo wa CCM kizimbani

**Na Allan Isaack,** ARUSHA

WAKAZI 25 wa Tarafa ya Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha wamefikishwa mahakamani, wakikabiliwa na shtaka la mauaji ya askari wa Jeshi la Polisi, G 4200 Koplo Garlus Mwita.

Washtakiwa hao, akiwamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Ngorongoro, Ndirango Laizer na madiwani tisa, walifikishwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha wakiwa chini ya ulinzi mkali wa Jeshi la Polisi.

Akisoma hati ya mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi, Herieth Mhenga, Wakili wa Serikali, Upendo Shemkole, alidai mahakamani huko kuwa, washtakiwa hao walitenda kosa hilo Juni 10 mwaka huu kwa kusababisha kifo cha Koplo Garlus.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri unaongozwa na Wakili wa Serikali, Upendo Shemkole, huku jopo la utetezi likiongozwa na Wakili, Jeremia Mtobesya.

Mawakili wengine wa utetezi ni Jebra Kambole, Joseph Ole Shangai, Peter Madeleka, Denis Mosses, Adolf Temba, William Ernest, Yonas Masiaya, Nicholous Ole Senteu, Samaito Mollel, Julius Lukumay, Ngeeyan Laizer, Deogratias Njau na John Lairumbe.

Wakili Upendo alidai shauri hilo limepangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini waliomba kubadilisha hati ya mashtaka ili waongeze shtaka moja.

Kutokana na ombi hilo, Mawakili wa Utetezi, Mtobesya na Madeleka, walipinga ombi hilo na wakidai limepelekwa kwa hatua ambayo siyo sahihi.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Upendo alidai mahakamani huko kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hivyo ipo kwenye hatua za upelelezi na walichowasilisha mahakamani ni kubadili hati na kuongeza kosa na kimsingi sheria haizuii mahali popote kubadili hati ya mashtaka.

Baada ya hoja hizo mahakama iliahirisha kwa muda kesi hiyo na baadaye ilirejea kwa ajili ya kutoa uamuzi mdogo.

Hakimu huyo alisema baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, mahakama inaruhusu kubadilisha hati ya mashtaka kwa kuwa hakuondoi haki yoyote ya washtakiwa hao.

Akiwasomea hati hiyo mpya ya mashtaka, Wakili Upendo alidai kosa la kwanza ni njama ya mauaji kwamba tarehe na sehemu isiyofahamika huko Ngorongoro, walipanga njama ya kuua maofisa wa serikali na maofisa wa polisi watakaoshiriki kuweka mipaka Pori Tengefu la Loliondo.

Alidai kosa la pili ni la mauaji kwamba Juni 10 mwaka huu, eneo la Ololosokwan, Wilaya ya Ngorongoro, kwa nia ovu, walisababisha kifo cha G 4200 Koplo Garlus Mwita.

Hakimu huyo aliwataka washtakiwa hao kutokujibu lolote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka kisheria kusikiliza shauri hilo na kesi hiyo iliahirishwa hadi Julai 14, 2022 itakapotajwa.

# Utenganishaji wa watoto pacha wafanikiwa MNH

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imefanikiwa kuwatenganisha watoto pacha walioungana baada ya kufanya operesheni iliyochukua takriban saa saba ikihusisha kutenganisha ini, mishipa mikubwa iliyomo humo pamoja na kuitenganisha ngozi iliyopo kwenye moyo.

Watoto hao ni Neema na Rehema ambao walizaliwa Septemba 21, 2021 kwa njia ya upasuaji wakiwa na kilo 4.9 wote kwa pamoja katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, ambao walipewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bungando) na baadaye Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jioni mara baada ya jopo la wataalam 31 kufanikisha operesheni hiyo, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto Hospitali ya Taifa Muhimbili, Zaitun Bokhary, alisema walianza kazi hiyo saa tatu asubuhi na kumalizika saa tisa alasiri.

"Katika operesheni hii, ugumu ulikuwa ni katika kutenganisha ini, watoto hawa walikuwa ini lao limeungana kabisa na kuwa kama kitu kimoja na kuna baadhi ya mishipa mikubwa katika ini ilikuwa imeungana kwa hiyo ilikuwa ni vigumu kutenganisha ini.

"Pia kwenye ngozi ambayo inafunika moyo ilikuwa imeungana na kufanya kitu kimoja wakati wa kutenganisha ilibidi ngozi ichanwe au ifumuliwe ili iweze kutenganishwa.

"Tunamshukuru Mungu tumeweza kutenganisha watoto hawa, kutenganisha ini na hatimaye kila mtoto akabaki na ini lake na mishipa mikubwa ya damu inayokwenda kwenye ini kila mtoto amebaki nayo," alifanua.

Dk. Bokhary alisema wameweza kufunika sehemu ya ngozi inayotumika kufunika moyo na sehemu ya mapafu.

"Watoto hawa walikuwa wameungana chini ya kifua kwa kiasi kikubwa pia ilituchukua muda kidogo kuweza kuzitenganisha sehemu za kifua na tumbo mwisho wa siku tumefanikiwa kuwatenganisha watoto hawa.

"Operesheni hii imehusisha madaktari wa upasuaji wa watoto wadogo (12), timu ya madaktari wa usingizi (6), madaktari wa kutengeneza uzuri (4), madaktari ambao kazi yao ilikuwa kushughulika na kuangalia mfumo mzima wa mtoto unakwenda vizuri (2), wauguzi (6), tulikuwa na timu ya kutosha iliyofanikisha upasuaji huu," alisema.

Mtaalamu huyo alisema kupitia upasuaji huo timu hiyo kwa ujumla imejifunza vitu vingi.

"Kama nilivyoeleza awali , changamoto kubwa ilikuwa ni ini kuwa kama moja katika kulitenganisha tunashukuru tulikuwa na mtaalamu kutoka Bahrain, Profesa Martin Corbally, ambaye ni daktari bingwa anayeshughulika na masuala ya mfumo mzima wa ini alikuwapo pale amesaidia sana.

"Hii imetupa changamoto zaidi kwa vijana wetu ambao sasa hivi wapo masomoni tuweze kuwapata wa kutosha kwa ajili ya kusomea upande huu," alisema.

Kuhusu kuungana, alisema hakuna sababu maalum wanayoweza kueleza kuwa imesababisha watoto kuungana ingawa kinadharia, wanapotaka kuungana kunakuwa na yai limerutubishwa lakini linashindwa kugawanyika kama kawaida na matokeo yake wanatoka wakiwa hivyo.

"Mzazi mwenye watoto walioungana tumboni hawezi kugundua, wito wajawazito wote ni vizuri waende kliniki kule watafanyiwa vipimo wakati wakiwa bado wajawazito, wanawake wengi tunaowapokea katika hospitali yetu, wanatoka pembezoni mwa Tanzania sehemu ambako, mama hajawahi kuhudhuria kliniki hata mara moja, anajifungua anapata watoto wameungana," alisema.

Profesa Corbally alishukuru kwa kushiriki katika operesheni hiyo ambayo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa kuwatenganisha pacha hao waliokuwa wameungana na kueleza kuwa itawachukua siku kadhaa kupata nafuu.

Upasuaji kama huo ni mara ya tatu kufanyika nchini ambapo wa kwanza ulifanyika mwaka 1994 ukihusisha watoto wawili wa kiume waliokuwa wameungana kwenye tumbo.

"Upasuaji wa pili ulifanyika mwaka 2018 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi tisa sasa na wanaendelea vizuri.

HABARI KITAIFA

# Mfanyakazi wa TANESCO afariki dunia akiwa 'gesti'

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MFANYAKAZI wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Katavi, amekutwa amefariki katika nyumba ya kulala wageni iliyoko Manispaa ya Mpanda mkoani humo.

Akizungumza na Nipashe jana, mfanyausafi wa nyumba hiyo, Tedi Moses, alidai kuwa mfanyakazi huyo alifika kwenye nyumba hiyo juzi jioni akiwa anaendesha pikipiki na kupewa chumba.

Alisema baada ya kupewa chumba, kuna mwanamke alikuja na kuingia kwenye chumba chake ambaye inadaiwa walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na kwamba baada ya muda, mwanamke huyo aliondoka na kumuacha mfanyakazi huyo chumbani huko.

"Huyo mwanamke alitoka akaniaga kuwa anaondoka, atarudi baadaye lakini hiyo baadaye hakurudi badala yake alirudi asubuhi. Sasa na mimi ilipofika saa tatu usiku niliondoka, nikaenda kulala, nimerudi asubuhi, nakuta watu wengi hapa, nilipouliza wakasema 'yule baba wa chumba namba nne (4) amefariki humu ndani," Tedi alisimulia.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ikulu, George Gadasi, alisema alipita asubuhi mtaa huo baada ya kuona watu wamejaa na alipohoji, aliambiwa kulikuwa na tukio la mtu kufia ndani ya nyumba hiyo.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, walimpigia simu mwenyekiti wa mtaa huo huku akidai chanzo cha kifo bado hakijafahamika.

Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi, Emmanuel Tinda, alikiri kuupokea mwili huo na kudai mfanyakazi huyo anakadiriwa kuwa na umri wa miaka kati ya 30 na 35.

Alisema waliupokea mwili huo ambao uliwasilishwa kwao na Jeshi la Polisi waliodai kuutoa nyumba ya kulala wageni inayofahamika kwa jina la Lake View na bado wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kudai kuwa mfanyakazi huyo alikuwa na



Mmoja wa wanachama wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Mary Mwita (aliyesimama), akitoa elimu ya ujasiriamali kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo mapema wiki hii, kwa lengo la kupunguza tatizo la ajira na ukatili unaosababishwa na umaskini wa kiuchumi katika jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliohusika upotevu mamilioni kikaangoni

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwachukulia hatua watumishi waliohusika na upotevu wa fedha za mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Sh. milion 378.

Mrindoko alitoa maagizo hayo jana kwenye kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo kilichojadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), akikabidhi orodha ya watu 18.

Hata hivyo, kati yao wawili wameshafariki dunia, hivyo kubaki na watuhumiwa 16 wanaopaswa kuchukuliwa hatua. Alisema fedha hizo zilikusanywa na watumishi mbalimbali pamoja na mawakala na baada ya kukusanya fedha hizo, hazikuwasilishwa sehemu yoyote wala kuingizwa kwenye mfumo wa serikali pamoja na muda kutolewa wa kuwasilisha fedha hizo.

"Kama fedha hazijaingizwa kwenye mfumo wa serikali, hazijaingizwa kwenye akaunti yoyote serikalini, maana yake fedha hizo zimeibwa na kwa kweli hatuwezi kuvumilia walioiba fedha za umma.

"Kwa hiyo, Kamanda wa TAKUKURU uje hapa mbele nikukabidhi orodha ili muwatafute, muwakamate na mfungule mashtaka mahakamani dhidi yao," aliagiza.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Katavi, Faustine Maijo, aliahidi kulifanyia kazi agizo hilo huku Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Katavi, Hassan Khalil, akisema halmashauri hiyo ilikuwa na hoja 79 zilizotolewa kwa mwaka 2020/21.

Khalil alisema halmashauri hiyo ilipata hati yenye shaka kutokana na mapato yaliyokusanywa kwa njia ya POS kutowasilishwa benki.

# Mapokezi ya gari la Royal Tour yafunika

**Na Waandishi Wetu**

MAPOKEZI ya gari aliloendesha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye uandaaji wa filamu ya Tanzania The Royal Tour, yamesimamisha shughuli kwa muda kwenye Viwanja vya Sabasaba, Dar es Salaam yanapoendelea maonyesho ya 46 ya kimataifa ya biashara, maarufu Sabasaba.

Gari hilo ambalo lilipelekwa jana kwenye banda la Maliasili na Utalii, lilikuwa kivutio kwa mamia ya watu waliojitokeza kwenye maonyesho hayo, baadhi wakilipiga picha na video na wengine kupiga nalo picha.

Baada ya kuwasili kwenye viwanja hivyo majira ya saa 4:45 asubuhi, lilipokelewa kwa gwaride maalum la askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na kuongozwa kwa gwaride hadi kwenye banda la Maliasili na Utalii.

Kaimu Kamishna Msaidizi wa TANAPA Kituo cha Dar es Salaam, Hassan Ngaluma, alisema wananchi watapata fursa ya kupiga picha na gari hilo ambalo lilitumiwa na Rais Samia kwenye programu ya Royal Tour.

"Gari hili liliendeshwa na Rais kwenye programu ya Royal Tour, litakuwa kwenye banda letu kama moja ya vivutio na wananchi watapata fursa ya kupiga nalo picha bure," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya maonyesho ya Sabasaba, gari hilo litapelekwa Hifadhi ya Taifa Serengeti ambako litaendelea kutumika kwenye masuala ya utalii.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii, Felix John, alisema lengo ni kuendeleza utalii nchini akisisitiza kuwa tangu filamu ya Royal Tour imefanyika sekta hiyo imepiga hatua.

"Wakati wa Covid ni kama sekta ya utalii ilishuka, lakini sasa imerudi kwenye kiwango kikubwa na filamu ya Royal Tour imechangia kwa kiasi kikubwa kukuza sekta ya utalii nchi," alisema.

Mapema jana, gari hilo lilitembezwa katika maeneo kadhaa ya Jiji la Dar es Salaam kabla ya kufika kwenye Viwanja vya Sabasaba.

Lilipita Daraja la Tanzanite, Morocco, Magomeni, Kariakoo, Kurasini hadi Viwanja vya Sabasaba.

# TRA yajizatiti elimu ya kodi Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema imejipanga kutoa elimu ya masuala mbalimbali kwa wananchi watakaokwenda kutembelea banda lao liliko katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF).

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam kwenye banda la taasisi hiyo, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, alisema elimu wanayoitoa inajumuisha namna ambavyo walipakodi hunufaika na misamaha ya kodi.

Alisema katika maonyesho hayo, wananchi pia watapata fursa ya kufahamu mambo mbalimbali ambayo yamefanyiwa maboresho na Bunge la bajeti la serikali kwa mwaka 2022/23, hasa kuhusu masuala ya kodi.

"Tunawaomba wawekezaji na wafanyabiashara wafike katika banda letu ili wapate elimu, mambo ni mengi sana ambayo tumepanga kuwaelimisha, kwa hiyo tunawaomba wasikose fursa hii," alisema Kayombo.

Pia aliwataka walipakodi na wananchi kwa ujumla waendelee kuwaunga mkono TRA ili wakusanye mapato kwa faida ya Taifa.

"Taifa linategemea ulipaji wa kodi wa wananchi ili liweze kufanya shughuli zake mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, hivyo unapolipa kodi, unakuwa umelisaidia Taifa lako," alisema Kayombo.

Alisema tayari timu maalumu ya wataalam ipo kwa ajili ya kupokea maoni ya wananchi sambamba na uwapo wa huduma ya kujisajili kwa mtandao.

"Katika maonyesho haya ya 46, TRA imekuwa ikitekeleza kaulimbiu inayosema 'mahali sahihi pa biashara na uwekezaji,'" alisema Kayombo.

# Wahofiwa kufa maji wakivusha ng'ombe

**Na Futuna Seleman**, RUFIJI

WATU watatu wanadaiwa kufariki dunia baada ya kuzama maji kwenye Mto Rufiji wakati wakijaribu kuvusha ng'ombe wa mfugaji kutoka Kitongoji cha Shaurimoyo, Kijiji cha Nyamwage, Rufiji mkoani Pwani kuelekea Kijiji cha Mtanange Aik.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi Protas Mutayoba, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotokea juzi majira ya saa tisa alasiri.

Aliwataja watu wanaodaiwa kupoteza maisha ni Mohamed Shamete, Juma Rwambo na Msafiri Makiyao waliokuwa wakishiriki kuvusha ng'ombe hao kupitia mto Rufiji ili wafike Ikwiriri kwa kusafirishwa kwenda Kijiji cha Dondo, Mkuranga mkoani Pwani.

"Walipofika katikati ya maji, yakawa mengi wakaanza kusukumwa hao ng'ombe na vijana wakakumbwa na mkondo huo wakapotea na ng'ombe wakaenda katika mkondo ambao siyo wenyewe.

"Ng'ombe 25 walipotea na ng'ombe 170 walioingizwa kwenye maji waliokolewa na wananchi na kwenda kuhifadhiwa sehemu maalum kwa ajili ya hatua zaidi kufanyika," alisema Kamanda Mutayoba.

Aliongeza kuwa jitihada zinaendelea kwa kushirikiana na wananchi na kamati ya ulinzi na usalama wilaya hiyo kwa pamoja katika eneo la tukio wakiangalia mbinu za kupata miili ya watu hao na maeneo ya mto unapoelekea wananchi wamepewa taarifa kama wataona miili imekwama ama inaelea majini, watoe taarifa ili taratibu zingine zikiwamo za kuiopoa na maziko zifanyike.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelle, akizungumzia tukio hilo, aliwasisitiza wananchi kuacha tabia ya kushirikiana na wafugaji kuvusha mifugo yao kwa kuwa jambo hilo ni hatari na wananchi wengi wanaliwa na mamba kutokana na wingi wa mamba kwenye Mto Rufiji.

"Ninawapa pole mliopoteza ndugu zenu, ninajua ni mipango ya Mungu lakini ninajua mnaweza kuepuka, nilishatoa maelekezo ng'ombe kutoka pointi moja kwenda nyingine wasiswagwe, magari yatumike kuwabebea kwani vifo vya kuliwa na mamba ni vingi hasa katika harakati za wananchi kuvusha mifugo bila kuzingatia taratibu," alionya.

Aliwataka wananchi kutojiamini kuogelea kwenye Mto Rufiji wenye mamba wengi kwa kuwa wanahatarisha maisha yao.

"Leo tumepoteza nguvu kazi, wameacha watoto, wameacha familia, nalikemea mara kwa mara jambo hili, tufike sehemu tuache kutafuta matatizo, usalama ni mdogo, sote tunajua kuna mamba," alionya.

Mmiliki wa ng'ombe hao na mkazi wa Handeni mkoani Tanga, John Mollela, alisema alikuwa akitokea Nangurukuru mkoani Lindi kuelekea Kijiji cha Dondo, Mkuranga mkoani Pwani na alipoka Rufiji, alikosa gari la kuwasafirisha ndipo alipofanya utafiti kutafuta njia za panya ili kuwavusha ng'ombe hao ili awahi kufika.

"Ng'ombe wawili waliliwa na mamba, mmoja kafa, ishirini walizama, nikalazimika kuwapa wananchi ng'ombe mmoja wachinje ili wanisaidie kuokoa ng'ombe waliokuwa wamenasa kwenye matope.

"Nilitozwa kila ng'ombe Sh. 300 kwa ajili ya kuvusha, walinieleza kuwa ipo sehemu inaitwa Mtanange ndipo wanakovushia ng'ombe," alisema.



Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), Kanali Shija Lupi (kushoto), akiangalia bidhaa zinazozalishwa na shirika hilo, alipotembelea banda la shirika hilo, katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam juzi. **Habari Uk. 7.** **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Vigogo TPA kizimbani kwa mashtaka uhujumu uchumi

**Na Grace Gurisha**

VIGOGO wanne wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka ya kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8, sawa na Sh. bilioni 4.2.

Washtakiwa hao ni: Peter Gawile (58), Ofisa Rasilimali Watu wa TPA na Mkazi wa Mianzini; Casmily Lujegi (65), mkazi wa Mbezi Juu na Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi wa TPA; Mashaka Kisanta (59), Mkurugenzi wa Idara ya Ununuzi; na Kilian Chale (51), Kaimu Mkurugenzi Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Mkazi wa Mbezi Makabe.

Akisoma mashtaka hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhan Rugemalira, Wakili wa Serikali, Timotheo Mmari, alidai kuwa washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu katika kesi ya uhujumu uchumi namba 38 ya mwaka 2022.

Mmari alidai katika shtaka la kwanza kuwa washtakiwa hao kati ya Oktoba Mosi, 2014 na Oktoba Mosi 2020 mkoani Dar es Salaam, walikula njama na kuisababishia TPA hasara.

Alidai kuwa kati ya Januari Mosi, 2015 hadi Februari 17,2015, washtakiwa wakiwa maofisa wa TPA, walitumia madaraka yao vibaya kwa kutangaza zabuni namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 kwa nia ya kujipatia dola za Marekani 1,857,908.04.

Ilidaiwa kati ya Oktoba Mosi 2014 na Oktoba Mosi, 2020 maeneo ya TPA na maeneo mengine ya Dar es Salaam, washtakiwa kwa makusudi walitangaza zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP).

Inadaiwa walitangaza zabuni hiyo bila kupata kibali cha Bodi ya Zabuni ya TPA na kushindwa kufuata kanuni za zabuni, hivyo kutoa malipo ya awali ya asilimia 40 bila idhini ya bodi hiyo, jambo lililosababisha TPA hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8.

Hata hivyo, mshtakiwa Madeni Kipande ambaye alikuwa Mkurugenzi wa TPA, hakusomewa mashtaka hayo kwa kuwa amefanyiwa upasuaji wa mgongo Muhimbili katika Kitengo cha Mifupa (MOI).

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo, bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi hadi itakapopata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchi (DPP).

Hakimu Rugemalira pia alihoji sababu za kuwaleta washtakiwa hao mahakamani wakati upelelezi hujakamilika. Alisema kesi ilipaswa kukamilika upelelezi ndipo washtakiwa wafikishwe mahakamani kwa lengo la kuanza kusikiliza.

Pia aliwataka washtakiwa kufanya maombi Mahakama Kuu kwa sababu kiasi cha fedha wanachodaiwa kusababisha hasara ni kikubwa na kwamba mahakama yake hiyo haiwezi kutoa dhamana kwao. Hakimu Rugemalira aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 14 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Mkurugenzi aingia matatani kukacha ziara ya mkuu mkoa

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, amepiga marufuku Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa zilizopo mkoani humo kutuma wawakilishi wao kama hakuna ulazima anapofanya ziara zake za kusikiliza kero za wananchi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kupata taarifa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, hakuwapo kwenye mkutano wa hadhara wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Misigiri, Kata ya Ulemo wilayani Iramba kwa ajili ya kusikiliza kero zao.

"Mkurugenzi yuko wapi? Hawa wananchi wakitoa kero, nani atazitatua? Ninamweleza RAS (Katibu Tawala wa Mkoa), RC (Mkuu wa Mkoa) ninapofanya ziara, wakurugenzi wawapo na kama kuna ruhusa, nijulishwe nafasi yake itawakilishwa na mtumishi mwingine.

"Hapa nina Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania ( TANROADS) ana kazi nyingi sana, nina Meneja Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), nina watu wa maji, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wapo hapa, ni kwa sababu tunataka kero zao wazisikilize moja kwa moja kutoka kwa wananchi," alisema.

Dk. Mahenge alisema yeye ni mwakilishi wa Rais, hivyo kero za wananchi Rais atazipata moja kwa moja kwa sababu wananchi wana haki ya kumweleza kero zao.

Alihoji kulikuwa na ulazima gani kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ua Iramba kwenda kuhudhuria mkutano wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) na kwanini asingetuma mwakilishi kwenda huko ili yeye ashiriki ziara.

"Marufuku DC (Mkuu wa Wilaya) na nipate maelezo kama hakukuwa na mtu mwingine wa kwenda huko mpaka aende yeye tu, hata aliyemwita alipaswa anieleze mimi Mkuu wa Mkoa kwamba tunajua una ziara lakini tunamwitaji DED tuone kama ni yeye tu ndo anatakiwa aende maana halmashauri ni taasisi," alisema.

Akizungumzia kero ya maji iliyotolewa na wananchi, aliiagiza RUWASA kwamba wiki ijayo wananchi wa Kijiji cha Misigiri waanze kuipata mara baada ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukamilisha kufunga transfoma ili mota za kusukumia maji zianze kufanya kazi.

Kuhusu elimu, aliwapongeza wananchi wa Wilaya ya Iramba kwa kuchangia fedha za chakula kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi 76 na za sekondari 25, hatua ambayo imesaidia wilaya hiyo kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba na kidato cha nne.

"Msingi wa mwanafunzi kufanya vizuri ni pale tu anapokuwa hana njaa akiwa darasani, ninawashukru wananchi wa Iramba kwa kuendelea kuchangia fedha za chakula," alisema.

Mkuu wa Mkoa aliwahidi wananchi hao kuwa kero zote walizoziwasilisha, serikali itazifanyia kazi. Katika ziara yake hiyo, kiongozi huyo aliongozana na wataalamu wa idara zote za serikali.

# Serikali yamwaga ajira zingine 1,600

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeajiri watumishi wapya 1,605 wa kada za afya zilizo chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Wizara ya Afya huku nafasi 16 za madaktari bingwa zikikosa waombaji.

Watumishi hao walioajiriwa ni madaktari, wafamasia, wateknolojia wa dawa, wateknolojia wa maabara, wateknolojia wa mionzi, wateknolojia wa macho, maofisa uuguzi, watoa tiba kwa vitendo, wazoeza viungo kwa vitendo, maofisa afya mazingira pamoja na wasaidizi wa afya.

Kwa mujibu taarifa iliyotolewa kwa umma juzi na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, nafasi zilizokosa waombaji, zitajazwa kwa mujibu wa kanuni na sheria za ajira katika utumishi wa umma.

Alisema waajiriwa hao wanatakiwa kuripoti katika ukumbi wa chuo cha uuguzi na ukunga Mirembe mkoani Dodoma ndani ya siku 14 kuanzia juzi wakiwa na vyeti halisi vinavyohitajika.

Alisema kwa yeyote atakayeripoti akiwa na nakala pungufu zinazohitajika, hatapokewa.

Alisema watumishi hao wapya wamepangiwa vituo vya kazi kwa kuzingatia uanzishwaji wa Hospitali mpya za Kanda Mtwara na Chato, Ujenzi wa Hospitali za Rufani za Mikoa.

"Pia upanuzi wa majengo mapya katika Hospitali za zamani (Sekou Toure (Mwanza),Mawenzi (Kilimanjaro), Maweni (Kigoma), Mbeya Mkoa na Kanda, Kibongoto, Mirembe (Dodoma). Mahitaji ya watumishi wanaohitajika katika Hospitali mbalimbali za Kanda, Maalumu na Mikoa ukilinganisha na wagonjwa wanaopata huduma," alisema.

Awali, alibainisha kuwa ajira hizo zilitangazwa mwezi Aprili, 2022 ambapo wizara hiyo ilipata kibali cha kuajiri wataalamu 1,650 wa kada mbalimbali ambapo kati ya hizo, nafasi 29 ambazo huzihusiani na afya moja kwa moja zitatangazwa na Sekretarieti ya Ajira.

Alisema katika nafasi 1,621 zilizobaki chini ya wizara hiyo, waombaji 19,464 ndiyo walikamilisha taratibu za uombaji kwenye mfumo huku waombaji 8,404 wakishindwa kukamilisha taratibu za uombaji.

"Kati ya waombaji 19,464 waliofanyiwa uchambuzi, waombaji 7,897 walikidhi vigezo vya awali kama vile kuzingatia miundo ya utumishi kwa kada za afya, waombaji walihitimu masomo yao kuanzia mwaka 2020 kurudi nyuma isipokuwa madaktari bingwa, wahandisi vifaa tiba, fundi sanifu vifaa tiba, wateknolojia na walemavu," alisema.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAARIFA KWA UMMA**

**USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI (EFDs) KWA WAFANYABIASHARA WOTE KATIKA ENEO LA MKOA WA KODI KARIAKOO**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu wafanyabiashara wote katika eneo la mkoa wa kodi Kariakoo kuwa wanapaswa kusajiliwa na kupewa namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015. ***Wafanyabiashara wote wanatakiwa kujisajili na kupatiwa TIN*** ndani ya siku kumi na tano (15) tangu tarehe ya kuanza kwa biashara husika.

Sambamba na hatua hiyo napenda kuwajulisha ***wafanyabiashara wote katika eneo la mkoa wa Kodi Kariakoo kuwa wanatakiwa kumiliki na kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFDs)***. Maelekezo haya yanatolewa kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi na yanalenga kuboresha usimamizi wa kodi katika eneo hilo ambalo ndio kitovu kikuu cha biashara nchini.

Kuanzia tarehe ya tangazo hili, mfanyabiashara atakayeendesha biashara yoyote katika eneo la Kariakoo bila kuwa na TIN na kutumia mashine ya kieleketroniki ya kutolea risiti (EFD) atakuwa ametenda kosa kisheria linalopelekea adhabu, kifungo au vyote kwa pamoja. TRA itaendesha zoezi maalum katika eneo la Mkoa wa Kodi Kariakoo kuhakikisha kuwa sheria na taratibu za uendeshaji biashara kama ilivyoelezwa katika Tangazo hili zinafuatwa.

Wafanyabiashara wote katika eneo la Mkoa wa Kodi Kariakoo wanahimizwa pamoja na maeneo yote nchini kuendelea kuzingatia sheria na taratibu za kodi ili kujiepusha na usumbufu usio wa lazima. Uzingatiaji wa sheria na taratibu za kodi ni msingi wa kujenga jamii ya walipakodi wazalendo wenye mchango mkubwa katika makusanyo ya Mapato nchini na hivyo kuchangia kwa vitendo jitihada za Serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo endelevu.

Kwa maswali, maoni, ushauri au taarifa zaidi tafadhali usisite kutembelea ofisi ya TRA iliyopo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia: Tovuti: **www.tra.go.tz** WhatsApp: **0744 23 33 33** Namba za Bure: **0800 750075, 0800 780 078 na 0800-110 016** Barua pepe: **huduma@tra.go.tz services@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

A. J. Kidata

**Kamishna Mkuu**

216928801

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zisajili kwa malengo

**DIRISHA** la usajili kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania, Championship, daraja la kwanza na Ligi Kuu ya Wanawake msimu wa 2022/2023 limefunguliwa rasmi jana na litafungwa Agosti 31.

Kikubwa kwa sasa ni kuanza kupitia yale mapendekezo ya mwalimu ambayo alitoa kuna yale majalada ya wakati ule wa usajili wa dirisha dogo mahali ambapo hapakukamilishwa basi pafanyiwe kazi.

Pia kwa mwendo ambavyo umekwenda tunaamini kwamba, kila baada ya mechi huwa kunakuwa na vikao vya kamati ya ufundi wanajua tatizo lipo wapi.

Zipo timu ambazo zimeanza kusajili wachezaji wapya na zipo ambazo zimeanza kuwaongezea mikataba wachezaji wao basi iwe ni kwa mapendekezo ya benchi la ufundi.

Yale masuala ya nina mchezaji wangu anajua sijui huyu atatusaidia muda wake umekwisha ni zamu ya benchi la ufundi kufanya kazi.

Ikumbukwe timu nne za juu zina tiketi mkononi ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao, michuano ambayo huandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Yanga ambayo ni bingwa wa Ligi Kuu ikifuatiwa na Simba ambazo zitawakilisha nchi kwenye michuano la Ligi ya Mabingwa Afrika, zinapaswa kuzingatia ukweli kwamba zisajili kwa mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi.

Hivyo, kutokana na wakongwe hao wa soka nchini, Simba na Yanga kuwa na uhakika wa kushiriki Ligi ya Mabingwa, zimekuwa zikihusishwa na wachezaji wengi.

Presha imekuwa kubwa kuanzia kwa mashabiki hadi viongozi wa klabu hiyo, kila mmoja akitaka kuona wanafanya usajili mkubwa wakuvutia kuelekea msimu ujao ambao miamba hiyo inaeleza kupania kufanya vizuri kimataifa.

Kutokana na presha hiyo, Nipashe tunaona kuna uwezekano ikawapoteza viongozi wa klabu na wote waliopewa jukumu la kufanya usajili, wakajikuta wakisajili kwa ushindani wa nani zaidi badala ya kufuata maoni na mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi ili mwisho wa siku waweze kutimiza malengo waliowekewa.

Tumelazimika kukumbusha hilo hasa kutokana na uzoefu mkubwa tulionao katika kipindi cha usajili hususan kwa klabu hizo mbili, ambazo huishia kushindana katika mbio za usajili na mwisho wa siku kujikutana zikisajili wachezaji wengi wa nafasi moja na kusahau mapendekezo muhimu kutoka kwa makocha wao.

Ikumbukwe pia nafasi za kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi ni 12 tu, ambazo ni chache sana, hivyo viongozi wa Simba na Yanga hawana budi kuwa makini kwa kusajili wachezaji katika nafasi muhimu ambao wanaona ni nadra kupata wazawa wakukidhi viwango wanavyohitaji.

Tunataka kuona wachezaji wanaosajiliwa kutoka nje wanakuja kutoa mchango mkubwa kwa klabu hizo na si kusajili wakuja kukaa benchi kutokana na kuzidiwa ama kuwa na ubora sawa na wazawa.

Hivyo, hiki si kipindi cha Simba na Yanga kuanza kukimbizana katika kuonyeshana jeuri ya fedha kuelekea dirisha la usajili, badala yake tunataka kuona kila klabu ikisajili kutokana na mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi ikiwa ni pamoja na wachezaji waliowafuatilia kwa muda mrefu.

Aidha, viongozi wa klabu hizo hawana budi kutumia vema nafasi hizo 12 kwa umakini mkubwa kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu huku wakimulika kwa umakini historia yao ya majeraha ili kuepuka wale wakucheza mechi moja inayofuata wanakuwa nje ya uwanja wakijiuguza kwa kipindi kirefu.


Tunaamini kama klabu hizo kongwe nchini, zitaacha mashindano katika mbio za usajili na kufuata kile ambacho mabenchi yao ya ufundi yamependekeza, zinaweza kupata wachezaji wazuri watakaowasaidia kwenye michuano ijayo ya kimataifa na kufika mbali.

Lakini lengo letu ni kuona usajili unaofanywa unakuwa wa tija na kuzaa matunda kwa angalau msimu huu tushuhudie timu zaidi ya moja zikitinga hatua ya robo fainali, nusu na hatimaye fainali kwenye michuano hiyo ya CAF, na hilo litawezekana tu kama zitatuliza kichwa kuelekea kipindi hiki cha usajili na si kusajili kwa mashindano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera TFF kuwahisha Ligi Kuu mapema

**KATIKATI** ya mwezi uliopita niliandika kwenye safu hii kulitaka Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kupitia Bodi ya Ligi kuanza ligi ya msimu ujao mapema.

Niliandika hivyo kutokana na kuwa na wasiwasi kuwa msimu ujao huenda Ligi Kuu ikachelewa kuanza.

Kwa sababu ya msimu huu ilichelewa kuanza na imechelewa pia kumalizika. Ilianza Septemba 27 na kumalizika Juni 29.

Nilitoa sababu za kutaka TFF kupitia Bodi ya Ligi kwanza kabisa kuisaidia timu ya taifa, Taifa Stars ili iwe sawa kwa ajili ya mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali AFCON zinazotarajiwa kufanyika mwakani nchini, Ivory Coast.

Ndiyo, kuisaidia kwa sababu baada ya kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Algeria na sare ya bao 1-1 dhidi ya Niger, Taifa Stars itacheza tena mechi yake ya tatu dhidi ya Uganda, Septemba 19 mwaka huu.

Sasa kama ligi ya msimu uliomalizika ilianza Septemba 27, basi mechi hiyo ingeweza kuikuta Stars ikiwa na wachezaji ambao hawajaanza ligi.

Ni kipindi ambacho wachezaji watakuwa bado hawako fiti, kwani wengi watakuwa wanajitafuta kwa sababu ya kutoka kwenye mapumziko marefu. Hata kocha jinsi ya kuchagua itakuwa shida.

Nikashauri tu angalau ligi ianze katikati ya mwezi Agosti, ili mpaka mechi ya Uganda inafika, tayari wachezaji wameshaanza kuchanganya, na hata unaweza kuwapata wachezaji wapya ambao wameonyesha viwango bora.

Kwa sababu hizi na zingine nitakazoziandika, nikaitaka TFF na Bodi yake kuangalia uwezekano wa ligi msimu ujao kuanza mapema kabla ya Septemba, vinginevyo tutakuwa tumeumia kwenye maandalizi ya kwenda AFCON.

Inawezekana kabisa kuwa mawazo niliyoandika kwenye safu ile yameonekana na majuzi Bodi ya Ligi imetangaza msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/23 utaanza Agosti 17 na kumalizika Mei 27 mwakani.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo akabainisha kuwa ligi ilichelewa kumalizika kutokana na janga la virusi vya corona.

Lakini nimkumbushe Kasongo kuwa siyo kuchelewa kumalizika, hata kuanza ilichelewa kwani si mara nyingi Ligi Kuu inaanza Septemba 27, badala yake huanza Agosti.

Na hii yote kama alivyosema ilisababishwa na ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Niwapongeze TFF na Bodi ya Ligi kwa kuwa wasikivu na kufanyia kazi mawazo au ushauri wote unaotolewa na wadau mbalimbali wa soka, wakiwemo waandishi wa habari, watangazaji na wachambuzi pia.

Kwa kuanza Agosti 17 mpaka kufika Septemba 19 ni mwezi mzima, hivyo angalau wachezaji watakuwa wameshajiunga na timu zao, wameshafanya mazoezi magumu ya kujenga miili yao kwa ajili ya purukushani za msimu mzima, lakini kizuri zaidi watakuwa wamesh-acheza angalau mechi mbili au tatu za Ligi Kuu. Hii inatosha sana kuwaweka vema na kwenye hali ya utimamu watakapokwenda kuitumikia timu ya taifa.

Pia kuanza kwa ligi mapema kutazisaidia timu nne za Tanzania zitakazokwenda kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Najua timu ya Simba itaanza kucheza Oktoba raundi ya kwanza na yenyewe ndiyo itakayonufaika zaidi kwa sababu itacheza mechi nyingi za Ligi Kuu hadi mwezi huo itakapoanza kampeni zake, lakini angalau timu za Yanga, Azam na nyingine itakayopatikana zitakuwa zimecheza mechi kadhaa za ligi kabla ya kuanza hatua ya awali.

Hii itazisaidia kwani wachezaji wao watakuwa wameshaanza kuzoeana na kupata mikiki ya ligi kabla ya kwenda kwenye michuano hiyo migumu.

Tuliona misimu kadhaa nyuma, ligi ilipochelewa kuanza na timu kuanza michuano ya kimataifa kabla ya ligi zikatolewa.

Simba ilitolewa na UD Songo ya Msumbiji kwa sababu ilicheza mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa ligi ya Tanzania ikiwa bado haijaanza, hivyo kuwa na tatizo la muunganiko na wachezaji kutozoeana.

Simba ilianza kucheza michuano hiyo, ikiwa ugenini Agosti 10, 2019, zikatoka suluhu na mechi ya marudiano ikapigwa Agosti 25, 2019 na kutoka sare ya bao 1-1, ikatolewa kwa goli la ugenini.

Ligi ya msimu huo ilianza siku ya pili baada ya Simba kucheza mechi ya marudiano Agosti 26, yenyewe ikianza kucheza Agosti 29 dhidi ya JKT Tanzania.

Ni mechi iliyowaumiza mno wanachama na mashabiki wa Simba, lakini ukiiangalia kiundani timu hiyo ilicheza bila kuwa na mechi sahihi ya ushindani kwa sababu ya kuchelewa kwa ligi.

Kwa hili ni lazima nitoe pongezi kwani Bodi ya Ligi na TFF si tu inaongoza soka, lakini inajali maendeleo yake, mawazo na maoni ya wadau pia.

# Raia wa Congo waadhimisha uhuru wakichangia damu

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kusherehekea miaka 62 ya Uhuru wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), raia wa nchi hiyo wanaoishi nchini, wameamua kusherehekea sikukuu hiyo kwa kuchangia damu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala.

Katibu wa Jumuiya ya Wakongo Wanaoishi Tanzania, Patriki Mbuyanzi, akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa juzi, alisema wamefanya hivyo ili damu iliyopatikana, isaidie kuokoa wagonjwa walioko hospitalini huko.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuonyesha mapenzi waliyonayo kwa Tanzania, akisisitiza wamekuwa wakiishi vizuri nchini bila bugudha yoyote na kujiona kama wako Congo.

"Leo (juzi) tunasherehekea kutimiza miaka 62 ya uhuru wetu lakini Tanzania kuna watu wengi wanafariki dunia kwa kukosa damu (hospitalini), hivyo tumeamua kusherehekea kwa kuchangia damu ili ikawe msaada kwa wenzetu na hata kwetu pia pindi tutakapopatwa na changamoto ya kupungukiwa damu," alisema.

Katibu huyo alifafanua kuwa hiyo haikuwa mara yao ya kwanza kufanya hivyo, akikumbusha kuwa ilikuwa mara ya tatu kwao kuchangia damu katika hospitali hiyo kongwe.

Mjumbe wa jumiya hiyo, Maua Faidha, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuboresha amani na mshikamano, hali inayofanya Wakongo wengi waliopo nchini kujihusisha katika biashara na kujiingizia kipato bila tatizo.

"Kuna kitu ninapenda kusema, siyo Wakongomani wote wanapenda muziki, siyo Wakongomani wote wanapenda vita, lakini nimshukuru Rais Samia kwa kutupatia vile vibali, tunadunda muda wote na tunaishi kwa amani sana tofauti na wale wasio na vitambulisho, ndio maaana wanashindwa hata kufanya biashara wakihofiwa kukamatwa," alisifu. Mwanajumuiya mwingine, Diom Bambeya, aliwaomba Watanzania kuendelea kuishi kwa amani na Wakongo waliopo nchini, akikumbusha kuwa hata Congo kuna Watanzania wanaoishi huko.

Daktari katika Kitengo cha Utoaji Damu cha hospitali hiyo, Ekinala Christopha, alisema wamefanikiwa kupata chupa 15 za damu katika harambee hiyo na kushauri watu wengine kuiga mfano huo mzuri.

"Tulikuwa na upungufu wa damu katika stoo yetu lakini leo (juzi) tumepata chupa 15 na bado wanaendelea kumiminika kutoa damu, hili ni jambo zuri.

"Damu hii itasaidia sana hasa kwa kinamama wanapojifungua, wanatumia damu nyingi sana, hivyo ninashauri Watanznaia na watu kutoka nchi zingine kuiga mfano huu," alihimiza daktari huyo.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ndatwa Ngwilabuzu (wa tatu kushoto), akipokea sehemu ya madawati, viti na meza vyenye thamani ya Sh. milioni 20, kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar, Donatus Richard, katika viwanja vya Shule Sekondari Buguruni Moto, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya shule tatu za sekondari za Buguruni Moto, Misitu na Umoja, Wengine ni Meya wa Jiji hilo, Omary Kumbilamoto (kushoto), Diwani wa Kata ya Buguruni, Bosoro Pazi (wa pili kushoto), na (wa nne kulia) ni Mkurugenzi wa Jiji, Jumanne Shauri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RAS ataka uadilifu fedha za TASAF

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Tawala Mkoa wa Pwani, Mwanasha Tumbo, amewataka waratibu na wasimamizi wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuhakikisha wanakuwa waaminifu katika kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Akizungumza jana wakati wa kikao kilicholenga kujadili shughuli za mpango huo, alibainisha yapo malalamiko kutoka kwa wanufaika kwamba wakati mwingine fedha hizo haziwafikii, akisisitiza kuwa jambo hilo linachafua mpango mzima wa utekelezaji wake.

"Malalamiko hayo yanajitokeza kutokana na kuwaachia watendaji na wenyeviti wa vijiji fedha na kusababisha fedha husika kuchelewa kuwafikia walengwa, ni lazima zisimamiwe ili kutimiza azma ya serikali na kujiepusha na migongano.

"Utaratibu wa sasa mnawatumia wanufaika fedha kwa njia ya simu, changamoto iliyopo walengwa wengine hawajui matumizi ya mitandao ya simu, anamwagiza mjukuu wake, jirani au jamaa hadi fedha ikitoka unakuta mlengwa anapata pungufu ama kunufaisha wasiostahili," alisema.

Mwanasha alisisitiza waratibu na wasimamizi wa fedha hizo kuangalia namna bora ya kutoa elimu inayoelekeza juu ya utaratibu huo ili wahusika wapate uelewa wa kutosha.

Mratibu wa TASAF mkoani Pwani, Roselyn Kimaro, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, zaidi ya Sh. bilioni 5.6 zimepokewa, eneo lao likiwa na kaya 29,683 zinazonufaika na mfuko huo kupitia mpango huo wa kunusuru kaya maskini.

"Tutahakikisha tunasimamia fedha hizo za mfuko kwa kuimarisha ukaguzi na tunaweka mikakati ya kuboresha usimamizi katika miradi inayoanzishwa na wanufaika ili ifikie malengo," aliahidi Roselyn.

# Wanafunzi waanzilishi wa Baobab wavutiwa mafanikio

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI waanzilishi wa Shule ya Sekondari Baobab iliyoko Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani, wameshangazwa na maendeleo ya miundombinu ya kisasa iliyojengwa katika shule hiyo.

Walibainisha hayo siku walipotembelea shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2005 kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tano na wao kuwa wanafunzi wa kwanza kabisa katika shule hiyo.

Mmoja wa wanafunzi hao waanzilishi, Irene Kamugisha, alisema wameshangazwa na mazingira mazuri ya shule pamoja na miundombinu walyoikuta tangu walipohitimu masomo miaka 14 iliyopita.

Alisema walianza masomo wakati shule haikuwa na miundombinu bora kulinganisha na ilivyo sasa.

"Kwa kweli tulipofika hapa tumeduwaa sana kwa sababu haya majengo hayakuwapo wakati sisi tunasoma. Ninawashukuru walimu na uongozi wa shule kwa kunipa elimu nzuri iliyoniwezesha kujiendeleza hadi kuwa mhasibu.

"Sasa hivi ninafundisha masuala ya usimamizi wa fedha kwa watu na kampuni mbalimbali," Irene alipongeza.

Mwanafunzi mwingine mwanzilishi, Lucyana Muro, alisema ameshangazwa na namna uongozi wa shule hiyo ulivyopiga hatua na kufanikiwa kujipanua kwa kujenga majengo mengi ikiwamo zahanati ya shule, maktaba ya kisasa, maabara, jengo jipya la utawala, kuanzisha mkondo wa wavulana na Shule ya Awali na Msingi Baobab.

Wanafunzi hao waanzilishi waliishukuru shule kwa kuwalea vizuri kimaadili na kuwapatia elimu bora iliyowasaidia kuendelea vyema na masomo ya elimu ya juu na hatimaye kuwa wataalamu katika nyanja mbalimbali kama vile uhasibu, uchumi, biashara, udaktari, nishati na gesi.

Pia walipeleka salamu kwa uongozi wa shule kutoka kwa mwanafunzi mwanzilishi mwenzao aitwaye Kissa Kasongwa ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Wilaya ya Njombe kwamba ameshindwa kufika kutokana na mwingiliano wa ratiba.

Meneja wa Shule hiyo, Sophia Mawenya, alisema shule ilianza ikiwa na wanafunzi 25 wa kidato cha kwanza lakini kadri muda ulivyokwenda, kasi ya wanafunzi ilizidi kuongezeka kutokana na ufaulu wa wanafunzi kuwa mzuri, hata kuweza kutoa wanafunzi bora kitaifa kwenye Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita. Alisema Dk. Jakaya Kikwete ndiye aliyeizindua rasmi shule mwaka 2007 akiwa Rais wa Tanzania na baada ya hapo, idadi ya wanafunzi ilizidi kuongezeka.

Aliwataka wanafunzi wa shule hiyo kusoma kwa bidii na kuwa na nidhamu nzuri kwa kuwa hakuna mafanikio yanayoweza kuja bila mhusika kujituma na kuwa na nia thabiti ya kufanikiwa.

Aliwaeleza wanafunzi wanaosoma sasa shuleni hapo kuwa wanapaswa kujifunza kutoka kwa wenzao waliosoma hapo na kupata mafanikio.

Aliendelea kueleza kuwa wanafunzi hao waanzilishi wana maisha mazuri kwa sababu walikuwa wanajituma katika kusoma na kuwa na nidhamu nzuri. Aliwaasa kuacha kuiga mambo wanayoyaona kwenye mitandao na runinga.

# Wabuni mfumo kulinda usalama abiria wa basi

**Na Elizabeth Zaya**

CHUO cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Songea, kimebuni mfumo wa kuimarisha usalama kwa gari za abiria.

Akizungumza na Nipashe katika banda la VETA kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), mwalimu wa umeme wa magari kutoka katika chuo hicho, Andrea Shayo, alisema mfumo huo una uwezo wa kutambua abiria ambaye hajafunga mkanda.

Alisema endapo kuna abiria hajafunga mkanda wakati gari limeanza kutembea, mfumo huo hutoa taarifa kwa dereva na namba ya kiti alichokalia.

"Mfumo huu husaidia kutoa taarifa kwa dereva na unaonyesha namba ya seat (kiti). Kwa hiyo inakuwa rahisi kumwelekeza abiria afunge halafu ndiyo safari iendelee," alisema Shayo.

"Tunaona mfumo huu ni mzuri kwa sababu endapo utatumika vizuri utasaidia kupunguza usumbufu kwa askari wa usalama barabarani ambao hulazimika kusimamisha gari za abiria hususani zinazokwenda masafa marefu kuingia ndani na kukagua ambao hawajafunga mikanda."

Pia, alisema utasaidia kupunguza idadi ya vifo ambavyo husababishwa na kutokufunga mikanda kunapotokea ajali.

"Badala ya askari kufanyakazi hiyo ya ukaguzi wa mikanda, kazi hiyo itafanywa na madereva wenyewe na kuokoa muda ambao hupotea barabarani kwa ajili hiyo ya ukaguzi," alisema Shayo.

Alisema lengo la kutengeneza mfumo huo ni kutaka ufundishwe kwenye vyuo vya VETA nchi nzima ili wanafunzi wanaohitimu wakasaidie kuelimisha wengine kwenye jamii.



Mkurugenzi wa Rasilimali Watu Vodacom Tanzania Plc, Vivienne Penessis (katikati), akikabidhi baadhi ya vitabu kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya watoto yatima ya Bethsaida ya Mpiji Magoe jijini Dar es Salaam, Hollness Moshi, ikiwa ni sehemu ya msaada wa viti 100, meza 100, vifaa vya kuzalisha umeme jua (solar power) 20 na vitabu 388, uliotolewa na wafanyakazi wa kampuni hiyo shuleni hapo, juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Udhibiti wa Hatari na Utii wa Sheria, Agapinus Tax (pili kulia) na baadhi ya wanafunzi wa Shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TARI yahamasisha mbegu mpya miwa

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kanda ya Kibaha, imetoa wito kwa wakulima wa miwa wanaoendesha kilimo hicho kwa kutegemea mvua, kutumia mbegu mpya zilizofanyiwa utafiti na taasisi hiyo kwa ajili ya kuongeza tija.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mratibu wa utafiti wa miwa taifa TARI Kanda ya Kibaha, Minza Masunga, wakati akizungumza na Nipashe kwenye maonyesho ya 46 ya Kitaifa ya Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema mbegu hizo mpya zimefanyiwa utafiti kwa ajili ya wanaoendesha kilimo kwa kutegemea mvua ni nne na ulifanyika kwa zaidi ya miaka 17.

Alisema tayari zimesajiliwa kwa ajili ya kutumika japokuwa wanatarajia kuzisambaza zaidi kwa wakulima kuanzia mwaka wa fedha ujao.

Alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuhimili ukame na kutoa mavuno zaidi kuliko inayotumika sasa.

Pia, alisema zina uwezo wa kuhimili mashambulizi na inaweza kuvunwa mara nyingi.

"Tunawashauri wakulima watumie hizi mbegu mpya kwa sababu zina tija zadi," alisema.

"Kwa mfano kwa ekari 2.5 unaweza kuvuna tani 55 hadi 123, endapo shamba litahudumiwa vizuri kwa kufuata vizuri masharti yanayotakiwa."

**"Tunawashauri wakulima watumie hizi mbegu mpya kwa sababu zina tija zadi," alisema.**

# Wakulima wa mahindi kunufaika bilioni 20/-

**Na Faustine Feliciane**

WAKULIMA wa zao la mahindi nchini wanatarajia kunufaika na fedha Dola milioni tisa (zaidi ya Sh. bilioni 20) zilizotolewa na Serikali ya Marekani kwa ajili ya kununulia chakula kwenye kambi za wakimbizi zilizoko mkoani Kigoma.

Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Msaada (USAID), limetoa fedha hizo kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa ajili ya kununua mahindi na mazao mengine kwa wakulima wa ndani kutoka mikoa mbalimbali.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya makabidhiano ya msaada huo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, alisema msaada huo mpya utaifanya WFP kutoa msaada wa chakula kwenye makambi ili kuokoa maisha ya wakimbizi 204,000 walioko kwenye kambi mbili za wakimbizi mkoani Kigoma.

Aidha, Balozi Wright ameitaka Serikali ya Tanzania kuhakikisha mahitaji yote ya kibinadamu ya wahamiaji wote wanaoishi katika mazingira magumu nchini yanafikiwa.

"Fedha hizi zinazotolewa kwa WFP zitatumika pia kuwanufaisha wakulima wa Tanzania kwa kuwa mazao yote yatanunuliwa na WFP kwa wakulima wa ndani, tunaipongeza sana Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuwahifadhi wakimbizi hapa nchini na kutoa ushirikiano mzuri kwa taasisi za kimataifa," alisema Dk. Wright.

Mkurugenzi Mkazi na Mwakilishi wa WFP nchini Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, alisema WFP imekabiliwa na upungufu mkubwa wa fedha tangu mwaka 2020 uliosababisha kupunguza mgao wa chakula hadi asilimia 68 chini ya mahitaji, hali iliyosababisha uhatarishi wa ulaji wa vyakula, lishe na afya ya wakimbizi.

"Mchango huu ni muhimu sio tu kwa sababu ya thamani ya chakula kwenda kwa wakimbizi, lakini kwa sababu ya matokeo chanya yatakayotokana na ununuzi wa chakula ndani ya nchi," alisema Sarah.

Alisema fedha hizo zilizotolewa zitatumika kununua tani 12,000 za mahindi ambayo yatasagwa na kuingizwa kwenye mzunguko wa ugawaji wa chakula kwa wakimbizi walioko kwenye makambi Mkoa wa Kigoma.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi Wizara ya Mambo ya Ndani, Sudi Mwakibasi, alisema serikali inaridhishwa na juhudi zinazofanywa na mashirika ya kimataifa kusaidia wakimbizi, Tanzania kufanikisha makubaliano ya kimataifa.

Alisema juhudi pia zinapaswa zielekezwe mahali wanapotoka wakimbizi ili kuweka ushawishi na mazingira mazuri kwa wakimbizi watakaotaka kurejea makwao kwa hiari.

"Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa katika kufikia makubaliano ya kimataifa hususani kwa wakimbizi," alisema Mwakibasi.

Mkuu wa WFP mkoani Kigoma, Nyanzobe Malimi, alisema Tanzania ina wakimbizi 270,000 huku walioko kwenye makambi wakifikia 204,000.



**HABARI DODOMA**

# NBS yapewa jukumu taarifa hali ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeagiza Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfumo wa kiutawala wa kukusanya taarifa za hali ya ulemavu nchini kama inavyofanyika kwa takwimu za vifo vya watoto wachanga na vifo vinavyotokana na uzazi.

Pia imewataka watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi ili serikali ipate takwimu zinazoakisi uhalisia na ambazo zitatumika katika kutunga sera na kupanga mipango na programu mbalimbali za maendeleo ambazo zitazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Jijini hapa juzi, Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, alitoa maagizo hayo wakati wa kongamano la watu wenye ulemavu lililoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na NBS.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alisema serikali inaendelea kuyapa kipaumbele na nafasi kubwa masuala ya watu wenye ulemavu kwa kuwajali na kuwathamini.

Alisema serikali imezingatia ushiriki wao katika hatua zote za utekelezaji wa zoezi hilo la kitaifa na ushiriki wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA).

Waziri Simbachawene alisema katika kutekeleza azma ya kuwatumikia watu wenye ulemavu kama sehemu ya Watanzania, serikali imeendelea kufufua vyuo vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu ambavyo kwa muda mrefu vilikuwa vimefungwa kutokana na changamoto mbalimbali, ukiwamo uchakavu wa miundombinu.

"Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi kwa watu wenye ulemavu, imekarabati Chuo cha Luanzari, Tabora ambacho kilifunguliwa na kuanza kufanya kazi mnamo Julai 2021 chenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 120," alisema Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwajali watu wenye ulemavu na kuwaamini katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema watahakikisha wale waliopata nafasi mbalimbali za uongozi, wanafanya kazi kwa bidii ili wasimwangushe na waendelee kuwaamini wengi zaidi kwani wanaweza.

"Ninampongeza Rais Samia kwa kutujali sisi wenye ulemavu, ameonyesha kutupenda na tunamhakikishia kuwa tutaendelea kumpa ushirikiano, tunaomba aendelee kutuamini na kutoa nafasi mbalimbali za uongozi na sisi tunamhakikishia kuwa hatutamwangusha, tutafanya kazi kwa bidii," alisema.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema lengo la kuandaa kongamano hilo ni kupeana misingi na faida ya zoezi la sensa ya watu na makazi kwa watu wenye ulemavu.

Alisema tangu maandalizi ya sensa yalipoanza mwaka 2018, serikali ilianza kushirikisha kundi la watu wenye ulemavu katika hatua mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha nao wanahesabiwa na Taifa linakuwa na takwimu sahihi za kundi hilo.

"Katika ya sensa ya watu na makazi ya itakayofanyika Agosti 23 mwaka huu, tumeweka maswali ya kutosha ambayo yatasaidia kupata takwimu sahihi zitakazosaidia serikali kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi na Taifa kwa ujumla.

"Hii ni sensa ya sita kufanyika nchini lakini chini ya uongozi wa serikali Rais Samia Suluhu Hassan, itahusisha kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu kuliko sensa zilizopita," alisema



Meneja Mwandamizi wa masuala ya ubia kutoka GGML, Manace Ndoroma, (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu uzinduzi wa kampeni ya GGM Kili Chalenge 2022, inayolenga kukusanya fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi. Kushoto ni Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wahimizwa kushiriki sensa mwezi ujao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKIWA umebaki mwezi mmoja kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi nchini, uongozi wa wajasiriamali mkoani Dodoma umewahimiza wajasiriamali kushiriki kikamilifu ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi zitakazosaidia kuweka mikakati, ikiwamo ya kuwezesha kundi hilo kwa mitaji na maeneo ya kufanyia biashara.

Katibu wa Wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa kundi hilo katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23 mwaka huu.

Alisema wajasiriamali wanapaswa kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa hiyo ili kuiwezesha serikali kupata takwimu itakazozitumia kuweka mikakati ya kuliinua kiuchumi kundi hilo.

"Wajasiriamali tunapaswa kushiriki kikamilifu ili kuhesabiwa na kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi ambazo zitaiwezesha kutuwekea mazingira wezeshi ya kufanyia kazi kama vile kututengea maeneo ya kufanyia biashara zetu kulingana na idadi yetu," alisema.

Dioniz alisema kama wajasiriamali hawatashiriki kwenye sensa hiyo, itakuwa vigumu kwa serikali kupanga mikakati ya kulisaidia kundi hilo kupata fursa za mitaji na kutengewa maeneo ya kufanya biashara kulingana na mahitaji yao.

"Takwimu za makundi haya yataiwezesha serikali yetu hata inapopanga bajeti zake, kuzingatia idadi yetu kama vile mikopo ya asilimia 10 kutoka halmashauri lakini pia ile inayotoka katika mifuko ya kuwezesha wananchi kiuchumi, itatolewa kulingana na mahitaji yetu bila kumwacha mtu.

"Lakini kama tutashindwa kupata takwimu hali itakuwa ngumu kwa kuwa wale ambao hawatahesabiwa watatumia rasirimali zilizopangwa kwa ajili ya watu wengine," alisema Dioniz.

Kadhalika, alilitaka kundi hilo la wajasiriamali nchini kujiunga katika vikundi ili kupata fursa za mikopo kutoka taasisi za fedha na mifuko ya kuwezesha wananchi kiuchumi iliyopo chini ya serikali.

Vilevile, aliipongeza serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya wajasirimali nchini pamoja na maslahi ya watumishi wa umma.

"Tunampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufanya kazi vizuri ikiwamo kuandaa bajeti inayojibu kero za wananchi wanyonge lakini pia kwa kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa kutoa nyongeza ya mishahara kwa asilimia 23.3 na kutoa ajira nyingi za kada ya afya na walimu nchini," alisema.

## Ataka hatua miradi chechefu, uchafuzi wa vyanzo vya maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema wizara yake imefanikiwa kuikwamua miradi chechefu ya maji 126, huku akiziagiza bodi za taifa za maji kuhakikisha zinafanya kazi kwa weledi ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Pia ameziagiza bodi za mabonde ya maji kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji ili kuongeza tija katika usimamizi wa rasilimali maji.

Aweso aliagiza hayo juzi jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa bodi ya nne ya taifa ya maji inayoongozwa na Mwenyekiti Mbogo Mfutakamba.

Alisema kwa sasa wizara inajivunia mafanikio makubwa katika sekta ya maji, hivyo angependa kuona bodi hiyo inakuja na ubunifu ikiwamo kuishauri wizara maboresho zaidi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.

Waziri huyo alisema wamefanikiwa kubadilisha wizara hiyo kutoka kuwa ya lawama na kuwa wizara yenye kutatua kero za upatikanaji wa maji, hivyo jitihada hizo zinapaswa kuendelezwa kwa utendaji kazi wa ushirikiano.

"Ni aibu na fedheha kuwa wizara ya lawama. Bajeti yetu imepitishwa kwa asilimia 100, hivyo tuchape kazi ionekane na kuleta tija kwa wananchi," aliagiza.

Alibainisha kuwa sasa ni muda mwafaka wa kuwa na mpango mkuu wa rasilimali za maji kwa wizara ambapo baada ya sensa ya watu na makazi kukamilika, watakaa na kupitia mipango mbalimbali ili kufanya maboresho.

Akizungumzia bodi za mabonde, Aweso alisema wanapaswa kuhakikisha wanaendelea na utendaji kazi wao vizuri ili kuongeza tija katika usimamizi wa raslimali za maji.

"Ninaziagiza bodi za maji za mabonde kufanya udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji, mchakato wa sheria uko mbioni kukamilika," alisema.

Alifafanua kuwa mipango ya matumizi ya maji ni muhimu katika ukuaji wa uchumi ili kuwa na rasilimali za maji endelevu na ndiyo maana anasisitiza udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya mazingira.

Aliipongeza bodi ya tatu kutokana kuwa imefanya kazi ya mfano na kuwafikisha walipo.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema lengo kubwa ni kumtua mama ndoo kichwani, hivyo bodi hiyo inapaswa kuvaa viatu vya bodi iliyopita kuhakikisha inafanya kazi kwa weledi ili wizara ya maji isonge mbele.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Antony Sanga, alisema lengo la yote wanayofanya ni kuwapatia wananchi maji safi, bora na salama.





# Majaji wapeana uzoefu kutekeleza haki Afrika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KONGAMANO la Majaji wa Mahakama za kikanda lililojadili masuala mbalimbali ya kimahakama, kisheria na haki za binadamu barani Afrika, limehitimishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Katiba na Sheria, Haroun Ali Suleiman.

Akizungumza wakati akifunga kongamano hilo la siku tatu lilofanyika Hoteli ya Verde mjini Zanzibar juzi, Waziri Haroun alisema washiriki wa kongamano wamejadili namna bora ya kutekeleza haki za binadamu katika nchi za Afrika.

Waziri huyo alisema anaimani kuwa baada ya majadiliano hayo, hakuna mtu atakaedhulumiwa na haki itatendeka katika huduma zote zikiwamo za kijamii, kisiasa na kiuchumi bila kuwapo ubaguzi.

Alisema kongamano hilo ni sehemu mojawapo ya kuimarisha utalii ambapo washiriki wake ni kutoka nchi mbalimbali za Bara la Afrika ambao baadhi yao ni kwa mara ya kwanza wamefika Zanzibar na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii.

Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Imani Daud Aboud, alisema majadiliano katika ngazi za majaji katika mahakama za kikanda na kimataifa katika Afrika ni muhimu kwa ajili ya kubadilishana uzoefu wa kazi na kufuatilia mabadiliko mengi yanayoikabili dunia hivi sasa.

Alisema maendeleo ya jamii hayawezi kupatikana bila ya kuwapo kwa misingi imara ya haki za binadamu na utawala bora ambayo yanatakiwa kutekelezwa na viongozi wa nchi za Kiafrika.

"Katika kongamano hili tumefaidika sana, tumebadilishana uzoefu namna ya kutatua changamoto na kuweka mikakati ya kuhakikisha uhusiano huo unajengeka na kuwa na kanzidata ya uamuzi ambayo itatumika katika mahakama zote," alisema.

Rais huyo pia alisema ushirikiano huo unatakiwa kuwa na msingi wa kisera na kupata bajeti kutoka serikalini na wafadhili ili kuendeleza mazungumzo na mijadala kama hiyo kwa ustawi wa mahakama na masuala ya haki za binadamu Afrika.

Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika ya Mashariki, Nestor Kayobera, alisema misingi ya sheria na utawala bora ni mambo ambayo yanatawala maisha ya binadamu ambayo yanatakiwa kuwekewa misingi madhubuti ili jamii kuwa huru na hakuna ukiukwaji wa haki za binadamu.



Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Daud Aboud (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kumalizika kwa kongamano la majaji wa Mahakama za kikanda, lilojadili masuala ya kimahakama, kisheria na haki za binadamu Barani Afrika, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Karafuu kupimwa kidijitali Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imesema karafuu yote itakayonunuliwa na Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) itapimwa kwa kutumia mashine ya kielektroniki ili kuepusha udanganyifu na kushusha ubora wake katika soko la dunia.

Waziri wake, Omar Said Shaaban, alibainisha hayo jana alipozungumza na watendaji wa huko Pemba pamoja na wafanyanyakazi na wakulima wa karafuu.

Alisema ZSTC mwaka jana katika msimu wa mavuno ya karafuu, ilipata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni tatu baada ya karafuu iliyonunuliwa kuwa na mchanganyiko wa taka nyingi.

Alisisitiza kuwa kuwapo mashine hizo kwa kiasi kikubwa kutasaidia kubainisha uchafu pamoja na karafuu ambazo hazina sifa na ubora unaotakiwa kuingia sokoni.

"Kuanzia sasa karafuu yote itakayonunuliwa na shirika itapimwa kwa kutumia mashine za kielektroniki ili kujua ubora wake na sifa na kuepuka udanganyifu unaofanywa na wakulima," aliagiza.

Alisema serikali itaendelea kununuwa karafuu kutoka kwa wakulima na kamwe zao hilo halitoingizwa katika soko huria.

Baadhi ya wakulima walioshiriki katika mkutano huo, walifurahishwa na uamuzi wa serikali kununua mashine za kielektroniki kwa ajili ya kuangalia ubora wa thamani, hatua ambayo itasaidia kudhibiti na kupambana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wakulima ambao siyo waaminifu.

"Nimefurahishwa na uamuzi wa serikali kununua mashine kwa ajili ya kuangalia ubora na mchanganyiko wa taka ambao unaweza kushusha thamani ya karafuu katika soko la dunia," alipongeza Juma Hamad, mkulima wa karafuu.

Mfanyakazi wa ZSTC, Hamadi Ali, alisema tayari wameanza kuzifanyia majaribio mashine hizo na kubaini ubora wake katika kutofautisha karafuu na taka ambazo hazistahiki.

# Makamu Rais asifu mchango wa BBC

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema kuanzishwa kwa Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) mwaka 1957, kulichangia nchi za Afrika Mashariki kuunganishwa pamoja katika kuendeleza jitihada za kudai na hatimaye kufanikiwa kupata uhuru.

Othman aliyasema hayo juzi alipozungumza katika uzinduzi wa Kongamano la Sherehe za Miaka 65 tangu kuanzishwa Idhaa ya Kiswahili ya BBC alipokuwa hoteli ya Golden Tulip mjini Zanzibar.

Alisema nchi ya Uingereza kupitia matangazo yake ya idhaa hiyo ya Kiswahili, ilitengeneza jukwaa muhimu kwa wakazi wa Afrika Mashariki ambalo lilisaidia kuwaunganisha vyema wananchi katika jitihada zilizozaa uhuru katika nchi mbalimbali.

Makamu wa Rais alisema kutokana na hatua hiyo, jukwaa hilo limetoa somo kubwa katika kukuza uhuru kwa kuwaeleza wananchi masuala mbalimbali yakiwamo ya siasa, uchumi, jamii na maendeleo kwa jumla.

Alisema kuwa kupitia idhaa ya Kiswahili, wanapashana habari na kuwapa uwezo wananchi wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na hatimaye kuchangia wananchi kuwa mahiri na wenye weledi mkubwa na wanaofahamu dunia inavyokwenda kuliko nchi nyingi za Afrika.

Othman alisema wazungumzaji wa Kiswahili kupitia idhaa hiyo, walipata faida kadhaa za kuelimishwa, kufundishwa na hivyo mchango wao kuwa mkubwa na muhimu na ni fahari kubwa kwamba waliosimamia mafanikio hayo ni wananchi wa Afrika Mashariki wenyewe.

Alisema Umoja wa Mataifa umeipa heshima kubwa lugha ya Kiswahili kwa kuitangaza Julai 7 ya kila mwaka kuwa siku ya Kiswahili duniani na kwamba jambo hilo ni heshima kubwa iliyotokana na wadau pamoja na mchango mkubwa wa matangazo ya BBC.

Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili ya BBC, Caroline Karobia, alisema licha ya vikwazo kadhaa vinavyovikabili vyombo vya habari, wamefanikiwa kuipasha jamii tarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya uchumi, siasa na maendeleo.

Rai yake ni kuwapo ushirikiano zaidi na uungwaji mkono kati ya wadau, zikiwamo mamlaka mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya vyombo vya habari.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE




# KABEBA BONGO FLEVA

## Bila yeye wasingekuwepo hadi sasa

MWANAMUZIKI Omari Mwanga, maarufu kama Marioo, amekuwa kama alama ya Muziki wa Bongo, nje ya mipaka ya Tanzania.

Marioo amebeba umaarufu mkubwa kutokana na nyimbo tamu na aina ya uimbaji wake ambao uko tofauti na wasanii wengine.

Je Marioo metoka wapi?

Kwa wasiomjua kiundani, mwanamuziki huyo ni miongoni mwa wasanii wachache wanaotoka ukanda wa Pwani, kwani amezaliwa eneo la Kibiti Mkoa wa Pwani.

Kwa upande wa elimu, Marioo aliishia kidato cha pili kutokana na wazazi wake kushindwa kumlipia ada. Hata hivyo alihamia Dar es Salaam na kuishi eneo la Kigogo.

Marioo alianza safari yake ya muziki kama mtunzi wa nyimbo akitunga nyimbo mbalimbali kwa mastaa wa muziki nchini kama 'Wasikudanganye' iliyoimbwa na HYPERLINK "https://sw.wikipedia.org/wiki/Nandy" \o "Nandy" Nandy, 'Unaniweza' ulioimbwa na HYPERLINK "https://sw.wikipedia.org/wiki/Jux" \o "Jux" Jux.

Pia ameandika 'Banana' ya Janjaro, 'Nampa Papa' ya Gigy Money, 'Nabembea' ya Ditto, 'Pambe ya Christian' Bella, 'Mchakamchaka' ya Shilole, 'Bado' ya Mwasiti na Billinas. Wimbo wake wa bia 'Bia tamu' umekuwa kama bendera ya ushindi, kutokana na kuimbwa na kila mtu, huku ikishinda tuzo za TMA kama wimbo bora wa mwaka 2021/2022.

Kwa upande wake, Marioo alianza kutoa wimbo wake wa kwanza "Dar Kugumu" mwaka HYPERLINK "https://sw.wikipedia.org/wiki/2017" \o "2017" 2017. Kisha aliendelea kuangusha vigongo kama 'Inatosha, Unanionea, AYA, Raha, Chibonge na Mama Aminah.

Kwa ujumla Marioo ni msanii pekee nchini ambaye ameubeba muziki wa Bongo Fleva, kutokana na kazi yake ya uandishi kuwa na nyimbo nyingi kali ambazo zinaendelea kutamba.

BASI SAWA

## Lydia Mwanza imemtendea



MWANAMUZIKI wa Injili anayekuja kwa kasi kutoka jiji la Mwanza, Lydia Onesmo, amerudi kivingine na wimbo wake mpya, Amenitendea.

Lydia, ameliambia BT kuwa anaendelea kuliwakilisha vizuri jiji hilo kutokana na huduma yake ya uimbaji kuvuka mipaka na kuenea nchini kote.

"Wimbo huu nimemshirikisha Derick Ndoge na ninashukuru mashabiki wameupokea vizuri na kufanya nizidi kuwakilisha Mwanza, nimeachia audio na video itafuata baadaye kidogo," amesema Lydia.


## Dorah awaumbua wauza sura



MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Dorah, amesema sekta ya filamu ni ngumu kwa watu wanaoingia kwa nia ya kutaka kuonyesha sura.

Msanii huyo amesema kama msanii atakuwa imara, mvumilivu na anayejitambua, kila kitu kwake kitakuwa rahisi pamoja na kuaminiwa na kila mtu.

"Hakuna kitu kigumu katika sanaa ya filamu kama mtu atajitambua na kuelewa nini anatakiwa kufanya, kama utaingia kwa nia ya kuuza sura kila kitu utashindwa na kuona sanaa mbaya," amesema Dorah.




# KING JUNIOR AWAONYA 'WANAOJIFANYA TAAHIRA'

MWANAMUZIKI wa hip hop, Junior Mlowo, maarufu kama King Junior, ametambulisha wimbo wake mpya Usijifanye Taahira' kama funzo kwa vijana wasioheshimu wazazi.

Akizungumza na BT, Junior amesema baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu ameamua kurudi katika jukwaa la muziki na ngoma hiyo ya kuelimisha.

Amesema yeye kama msanii msomi, hapendi kuimba nyimbo za kusifu mapenzi na badala yake ameegemea nyimbo za kuelimisha pekee ambazo wengi hawafanyi.

"Usijifanye taahira ni wimbo unaowaonya vijana wasiokuwa na heshima kwa wazazi na jamii kwa ujumla kwa makusudi tu. Ni lazima sisi wasanii turudi katika nyimbo za aina hii ili kurudisha maadili yaliyopotea," amesema.

# Amaria: Anayeua kwa upanga atauawa nao

**Na Adam Fungamwango**

'AMARIA', ni filamu inayoonyesha jinsi jamii zetu zinavyoweza kuingia kwenye mzozo au ugomvi na jamii, familia au jirani.

Ugomvi huo unaweza kutokana na vitu vilivyo dhahiri au vilivyojificha vinafanyika bila wenyewe kufahamu.

Wapo watu wanaongizwa kwenye mgogoro bila wao kujijua.

Imechezwa na baadhi ya wasanii ambao ni Shukurani John, Hans Popa, Abdul Khalfan, Kassim Mbwembwe, Elizabeth Kombe, Mrs Ngokwe, Sweet Balih, Lucy Habaru, Jasmine Waziri na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa kijana Nyayo ana uhusiano wa kimapenzi na msichana Amaria kwenye kijiji fulani hivi.

Inavyoonekana ni kama wazazi wa pande zote mbili walikuwa hawapendi uhusiano wa watoto wao. Ikawa ni kupigana mikwara tu. Kila mzazi wa mmoja anapokutana na mkwewe anampiga mkwara kuwa na uhusiano na mwanaye.

Amaria anapata ujauzito. Anapoupata tu, Nyayo anabadilika. Hamtaki tena Amaria. Amaria anaumia na kuteseka, kwani ana kiumbe tumboni, lakini pia mpenzi wake amemkataa.

Mama Amaria, Bi. Ndoza anakasirika sana juu ya binti yake kupewa ujauzito na kutelekezwa. Anaahidi kulipa kisasi.

Nyayo anatangaza ndoa na mwanamke mwingine. Siku ya ndoa ndiyo inakuwa siku ya maafa, kwani mama yake anakufa kwa kurogwa na mama Amaria.

Halafu bwana harusi naye anakufa kutokana na husuda ya mama Amaria anayelipiza kisasi.

Kijiji sasa kinaanza kutafuta mtu anayefanya matukio hayo. Anakuja mama mmoja ambaye anakuja kumaliza utata.

Mama huyo ndiye mkuu wa uchawi kwenye kijiji jirani. Anafichua siri kuwa mama Amaria alifika kwake zamani kusaka uchawi, akapewa masharti uzao wake wa kwanza aupeleke huko, lakini hakutekeleza, kwani baada ya kumzaa Amaria hakufanya hivyo.



Na kama haitoshi uchawi huo akautumia kwa manufaa yake, hivyo anafaa kuadhibiwa na Amaria akijifungua mtoto atachukuliwa kufidia masharti yaliyowekwa.

Habari nzuri ni kwamba Nyayo na mama yake hawakufa, ila walichuliwa kiuchawi, hivyo wakarudishwa, Bi. Ndoza aliadhibiwa hapo hapo kwa kuchomwa moto akiwa hai.





# Ali Kiba huyoo Marekani

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva na CEO wa King Music Records, Ali Kiba, sasa rasmi ataanza ziara yake ya kutangaza albam yake ya Only One King.

Akieleza kupitia Instagram, Kiba amesema mwaka wake wa nne hajawahi kufanya shoo Marekani, hivyo imemfanya kuona umuhimu wa kwenda huko kutoa burudani.

Ameongeza kuwa tour hiyo itakuwa maalumu kwa ajili ya album yake, itawafanya mashabiki wake kufurahia kutokana na kazi atakayoionyesha.

# WA 5 HUKU MSONDO, HUKU SIKINDE

**Na Adam Fungamwango**

MSONDO na Sikinde ni bendi zenye mashabiki wengi nchini waliogawanyika pande mbili kama zilivyo timu za mpira wa miguu za Simba na Yanga.

Kila upinzani una historia yake. Msondo ilianzishwa mwaka 1964 na Chama cha Wafanyakazi Tanzania na kuiita NUTA Jazz Band, ikitumia mitindo mbalimbali na baadaye Msondo Ngoma.

Ilikuwa ikibadilisha majina ya bendi kulingana na siasa za nchi, hasa Chama Cha Wafanyakazi kilivyokuwa kikijibadilisha majina.

Ndiyo maana baadaye ikaitwa JUWATA Jazz Band, OTTU Jazz Band, TFTU Jazz Band na baadaye wakachukua jina la mtindo na Msondo Ngoma ndiyo ikawa jina la band na hii ni baada ya wanamuziki kujitoa kwenye Muungano wa Vyama Vya Wafanyakazi na kujitegemea wenyewe.

Upinzani wao na Sikinde ulioanza mwaka 1978, baada ya baadhi ya wanamuziki wa Msondo wakiongozwa na Muhidini Mwalimu Gurumo na kwenda kuanzisha Mlimani Park Orchestra, hapo ndipo ukaanza upinzani kati ya bendi hizo mbili.

Leo tunawaangazia baadhi ya wanamuziki nyota ambao wamewahi kupigia bendi zote mbili hasimu.

**Muhidini Mwalimu Gurumo**

Alikuwa mmoja wa viongozi wa Juwata Jazz, lakini aliondoka mwaka 1978 na kwenda kuunda Sikinde. Na ni mmoja wa wanamuziki waliosababisha upinzani mkubwa kati ya bendi hizo mbili.

Gurumo aliyefariki 2014, ni nembo ya bendi zote hizo mbili kwani hata majina ya Msondo na Sikinde ni yeye ndiye aliyeyabuni.

**Hassan Rehani Bitchuka**

Alikuwa mwimbaji tegemeo wa sauti ya kwanza kwenye bendi ya Msondo Ngoma.

Hata alipohama Gurumo mwaka 1978, Msondo ilionekana kutotetereka kwa kutoa vibao vingine vikali kama 'Sogea Karibu' na 'Uzuri si Shani'.

Hata hivyo, Sikinde iliwapa pigo Msondo mwaka 1979, ilipomchukua Bitchuka na kuacha kilio kikubwa.

Baada ya miaka 11, Bitchuka alirejea tena Msondo akiwa pamoja na swahiba wake Gurumo.

**Shaaban Dede**

Baada ya kuhangaika kwa muda mrefu kumpata mtu atakayeweza kufanana sauti na Bitchuka, hatimaye Msondo walimpata mwimbaji wa aina hiyo kutoka Dodoma International, Shaaban Dede.

Huyu alituliza kidogo mizuka ya mashabiki wa Msondo Ngoma kutokana na sauti yake kuwa na mfanano na Bitchuka.

Hiyo ilikuwa mwaka 1979. Lakini kama kawaida ya Sikinde. Huenda ilikuwa ina mikakati ya kuidhoofisha Msondo, kwani mwaka 1982 ilimchukua pia Dede na kuwaacha viongozi na mashabiki wa Msondo wasijue la kufanya. Ni mwanamuziki aliyerudi Msondo mara mbili, hivyo kuipigia kwa vipindi vitatu hadi alipofariki Julai 2017.

**Fresh Jumbe**

Akitokea Tanga, alichukuliwa na Marijani Rajab kwenye bendi ya Dar International, lakini muda mfupi tu akanyakuliwa na Msondo Ngoma. Hiyo ilikuwa ni miaka ya '80.

Akaingia na vibao kama 'Ama Zake Ama zangu' na 'Pamela' zilizompa umaarufu mkubwa.

Mwishoni mwa miaka ya '80 alichukuliwa na Sikinde na kutoka vibao kama 'MV Mapenzi no 2', 'Ramadhani', na nyingine nyingi ambazo aliimba kwa ustadi mkubwa.

Huyu naye anaingia kwenye orodha ya wanamuziki waliowahi kupigia bendi hizo mbili hasimu.

Kwa sasa yuko nchini Japan akiendelea na mambo ya muziki.

**Suleiman Mwanyiro**

Ni mpiga besi ambaye awali alikuwa akipiga kwenye bendi maarufu za taarabu Tanga, Black Star na Lucky Star.

Alichukuliwa na Msondo miaka ya '70 na kufanya kazi kwa umahiri mkubwa hadi alipokuwa mmoja wa wanamuziki walioihama bendi hiyo na kwenda Sikinde.

Naye pia alikuwa mmoja wa mlolongo wa wanamuziki waliokuwa wakihama na kurejea tena, kwani miaka ya 2000 alirejea tena Msondo na kutunga vibao vikali kama 'Kauka Nikuvae', 'Sekuntoza Kigudi Chauma', 'Tuelewane Mke wangu' na nyingine nyingi, kabla ya kuelekea tena Sikinde. Alifariki mwaka 2004.



# R Kelly kala matunda yake

MWANAMUZIKI mkongwe Marekani R.Kelly, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kujihusisha na unyanyasaji wa kingono.

Mwimbaji huyo alipatikana na hatia ya shtaka moja la ulaghai na makosa manane ya kukiuka Sheria ya Mann, ambayo inakataza usafirishaji wa mwanamke au msichana yeyote kwa madhumuni ya uasherati.

Kulingana na mtandao wa PageSix, ilichukua walalamikaji wanaume saba na wanawake watano saa tisa kupata haki katika siku mbili za kutoa uamuzi huo.

Waendesha mashtaka wa kesi hiyo walikuwa wamemtaka hakimu huyo atoe kifungo cha zaidi ya miaka 25.

Waendesha mashtaka pia walisema alitumia hadhi yake kama mtu mashuhuri na mali, kuwarubuni wanawake, pamoja na wasichana na wavulana wenye umri mdogo kushiriki ngono.



## Funke, JJ Skillz kisicho riziki hakiliki

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood Funke Akindele na mume wake Abdul Bello, maarufu JJC Skillz wamevunja rasmi ndoa yao.

JJC Skillz alifahamisha wafuasi wake kupitia ukurasa wa Instagram, akisema yeye na mke wake Funke wametengana.


"Wapendwa marafiki na familia nahitaji kuwajulisha kuwa mimi na Funke tumetengana. Tulishiriki mambo mengi pamoja na tumepata watoto wawili wazuri. Miaka miwili iliyopita imekuwa migumu sana kwetu," aliandika.

## Mali ya Chadwick yagawanywa

MKE na wazazi wa mwigizaji wa filamu ya Fallen Black Panther, Chadwick Boseman, wamefikia makubaliano ya mgawanyo wa mali zake baada ya kufariki dunia.

Taylor Simone na wakwe zake Leroy na Carolyn Boseman, watagawana sawa mali ya nyota huyo iliyofikia dola milioni 2.3.

Muigizaji huyo alifariki baada ya kuugua saratani iliyomuanza 2020, na kifo chake kimeleta majonzi kwa wapenzi wa filamu hiyo.





## Prince Harry, Meghani wateta kwa Oprah

MWANAMFALME wa Uingereza Prince Harry na mke wake, Meghan wamemtembelea mtangazaji mkongwe wa Marekani, Oprah Winfrey.

Wawili hao walionekana wakiingia kwenye jumba la kifahari la Oprah Jumamosi iliyopita na kutumia saa moja. Jumba hilo lina thamani ya dola milioni 100 za kimarekani.

Prince Harry na Meghan Markle walifunga ndoa mnamo 2018 kwenye harusi iliyojaa nyota mbalimbali, hata hivyo haijajulikana ni kwanini wanandoa hao walitembelea mtangazaji huyo.

## Osinachi sasa ni historia

HATIMAYE mwili wa mwimbaji wa nyimbo za Injili nchini Nigeria, Osinachi Nwachukwu, umezikwa.

Mwili wa mwimbaji huyo uliwasili katika mji wa nyumbani kwao wa jamii ya Amakpoke Umuaku, katika Jimbo la Abia na kuzikwa.

Nwachukwu aliaga dunia katika hali ya utata Aprili 2022 na kusababisha mume wake kufunguliwa mashtaka ya mauaji.

Kifo chake kilisababisha ndugu, wafanyakazi wenzake na rafiki zake kumnyooshea vidole mumewe, Peter Nwachukwu, huku wakimtuhumu kuhusika na kifo cha nyota huyo.



# UVCCM wanapojitosa kampeni za sensa 2022

Na Sabato Kasika

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umezindua rasmi kampeni za kuhamasisha watu kujiandaa kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi, inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa wa kwanza kwa Katibu Mkuu wa Taifa, Kenani Kihongosi, kufanya ziara ya kuhamasisha watu kujitokeza kuhesabiwa.

Katika ujumbe wake alioutoa katika viwanja vya Mwembe Yanga, Katibu huyo anawataka UVCCM kuingia mitaani kuelimisha vijana wenzao na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa sensa, ili kila mtu ajiandae kuhesabiwa.

"Tumezindua kampeni hizi mkoani Dar es Salaam, tutakwenda mikoa yote ya Bara na Visiwani, hivyo vijana watakuwa na kazi ya kuhamasisha na kutoa elimu ili watu wajiandae kuhesabiwa," anasema Kihongosi.

Anasema, kwa sasa wanajipanga kwenda mikoa ya kanda ya ziwa na kisha wataendelea kwingine ili kuhakikisha kampeni hizo zinafanyika nchi nzima .

Kihongosi anasema, ni muhimu vijana wa CCM kushirikiana na serikali yao kufanikisha zoezi hilo, kwa sababu hakuna tija kuendelea na idadi ya watu inayotokana na kukisia.

"Tutakanyaga maeneo yote yanayohusu umuhimu wa sensa, ili kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa tayari kuhesabiwa siku ikifika, " anasisitiza

**NINI MAANA YA SENSA?**

Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dk. Albina Chuwa anasema, Sensa ya Watu na Makazi ni moja ya zoezi muhimu linalokusanya taarifa za kila mtu aliyelala ndani ya mipaka ya nchi, usiku wa kuamkia sensa.

"Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo sensa zilizopita, itahusisha makarani wa sensa ambao watatembelea kaya zote nchini na kufanya mahojiano ya ana kwa ana na kati ya karani wa sensa na mkuu wa kaya," anasema Dk. Chuwa.

Anaongeza kuwa, ikiwa mkuu wa kaya hatakuwapo, karani wa sensa atafanya mahojiano na mtu mzima yeyote katika kaya ambaye ana taarifa za kutosha kuhusu kaya na wanakaya wenzake waliolala katika kaya husika usiku wa kuamkia siku ya sensa.

Anafafanua kuwa lengo la sensa ni kupata taarifa za kidemografia, kijamii na hali ya mazingira ili kupata takwimu sahihi zitakazoiwezesha serikali na wadau wengine kupanga kwa usahihi mipango ya maendeleo ya watu wake.

Kwamba hatua hiyo itasaidia katika sekta mbalimbali za elimu, afya, hali ya ajira, miundombinu kama barabara, nishati na maji safi, ambapo kwa msingi huo, sensa ni zoezi muhimu ambalo kila mtu anatakiwa kushiriki.



Baadhi ya vijana wa UVCCM Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa kwenye uzinduzi wa kampeni za kuhamasisha sensa. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

"Iwapo kila mtu atashiriki, sensa itakuwa ya mafanikio na itaisaidia serikali kutimiza wajibu wake kwa wananchi kulingana na idadi ya watu ya eneo husika ikiwa kama msingi mkubwa wa ugawaji wa keki ya taifa kwa kila eneo la utawala hapa nchini," anasema.

**ANAYETAKIWA KUHESABIWA**

Dk. Chuwa anawataja walengwa wa sensa hiyo kuwa ni watu wote watakaolala ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia ndani ya kaya na kaya za jumuiya kama vile hotelini, nyumba za kulala wageni na hospitalini.

Anataja maeneo mengine ambayo watu watahesabiwa usiku wa kuamkia sensa ni gerezani, katika mabweni ya wanafunzi, kambi za jeshi, vituo vya kulelea watoto wenye mahitaji maalum kama yatima na wazee.

"Maeneo mengine ni kambi za wavuvi, watu wasio na makazi maalum na vituo vya usafiri wa umma kama stendi za mabasi, viwanja vya ndege na bandari ambapo watahesabiwa kwa utaratibu maalum utakaoandaliwa na Kamati ya Sensa katika ngazi ya mtaa, kitongoji na shehia," anasema.

Alibainisha kuwa, taarifa za kidemografia (umri, jinsi, hali ya ndoa), taarifa za ulemavu (aina ya ulemavu na chanzo cha ulemavu). Taarifa za uhamaji, taarifa za vitambulisho vya utaifa na uhai wa wazazi.

Anaongeza kuwa kuna taarifa za elimu, shughuli za kiuchumi, umiliki wa ardhi na TEHAMA, hali ya uzazi, vifo na vifo vitokanavyo na uzazi, nyumba ikiwa ni hali ya umiliki wa nyumba, vifaa na rasilimali na udhibiti wa mazingira.

Anasema, kutakuwa na taarifa za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu, mipango ya TASAF, majengo, anuani za makazi, huduma za jamii katika ngazi ya kitongoji na mtaa, na kwamba taarifa zitakuwa ni za siri.

"Kama ambavyo hufanyika katika sensa na utafiti mwingine wa takwimu, kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu sura ya 351, taarifa zitakazotolewa kwa karani wa sensa zitakuwa ni siri," anasema.

Anafafanua kuwa zitatumika kwa madhumuni ya kitakwimu pekee, na kwamba kwa mujibu wa sheria hiyo, kila karani wa sensa atasaini kiapo cha kutunza siri za taarifa zote atakazokusanya.

"Chini ya kiapo hicho, hatakiwi kutoa taarifa alizotumwa kukusanya kwa mtu yeyote zaidi ya kuziwasilisha kama zilivyo katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar," anasema.

Kwamba, karani yeyote akithibitika kwenda kinyume na kiapo cha kutunza siri, atashtakiwa na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria hiyo.

**UNACHOTAKIWA KUFANYA**

Katika kufanikisha sensa, Mtakwimu huyo anasema, ni kila Mtanzania kumpa ushirikiano karani wa sensa atakapotembelea katika kaya, kwa kujibu maswali yote kwa usahihi atakayoulizwa.

"Ukiulizwa swali hujalielewa au hujalisikia vizuri, unayo haki ya kumuomba karani arudie kuliza au kutoa ufafanuzi ili uweze kutoa jibu kwa usahihi kulingana na swali lililoulizwa," anasema.

Anasema, kujibu maswali ya sensa ni matakwa ya kisheria, kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu sura Namba 351, na kwamba ni kwa mkuu wa kaya kuhakikisha anachukua taarifa zote muhimu kama umri, jinsi na hali ya ndoa.

Dk. Chuwa anasema, hatua hiyo inahusisha umiliki wa vitambulisho vya taifa, shughuli za kiuchumi za watu wote waliolala katika kaya usiku wa kuamkia siku ya sensa ili aweze kukumbuka wakati karani atakapomtembelea.

"Karani wa sensa akiongozana na Mwenyekiti au kiongozi wa serikali ya mtaa/shehia, atafika katika kaya akiwa na kitambulisho cha karani wa sensa na dodoso la sensa lililowekwa kifaa cha kielektroniki kiitwacho kishikwambi, (Tablet), na kuuliza maswali ambayo yatajibiwa na mkuu wa kaya," anasema.

Anafafanua kuwa, ikiwa mkuu wa kaya hayupo, mtu mwingine yeyote mzima katika kaya ambaye ana taarifa za kutosha kuhusiana na kaya na watu wote waliolala ndani ya kaya husika usiku wa kuamkia siku ya sensa, anaweza kujibu maswali ya sensa kwa niaba yake.

Mtakwimu huyo anagusia ugonjwa wa UVIKO-19 siyo kikwazo kwa yeyote kushiriki kwa nafasi yake, katika sensa ya mwaka huu, kwa kuwa kulingana na maendeleo ya ugonjwa huo, makarani na watendaji wote wa sensa watazingatia tahadhari zote zinazoelekezwa na wataalum wa afya.

"Lengo ni kuhakikisha hawaambukizi wananchi au wao kuambukizwa na wananchi wakati wa zoezi la sensa. Sensa kwa Maendeleo, kila Mtanzania ajiandae kuhesabiwa," anasema.



Katibu wa UVCCM Taifa, Kenani Kihongosi akizungumza alipozindua kampeni za kuhamasisha sensa jijini Dar es Salaam.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Enzi za unga wa Yanga, maduka ya kaya

## ●Chenga zinapikwa wali, zinasagwa tena
## ●Sukari guru, chai majani humo humo

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita kwenye makala iliyohusu majiko ya zamani, kuni, mkaa, mchina na stovu, nilipokea simu na meseji nyingi kutoka kwa watu mbalimbali wakikumbuka jinsi walivyoyatumia.

Mmoja akaaongeza kuwa jiko la stovu kwenye kupampu kama mafuta hayapandi juu, basi kuna sindano iliyotumika kuzibulia. Akaongeza kama huna, basi walitumia waya nyembamba kufanyia kazi hiyo.

Mwingine akasema mjomba wake alikuwa anamiliki lingo la miti ambalo pia alikuwa anauza kuni.

Yupo aliyezaliwa makala hii ya leo, ambaye alisema majiko hayo yalitumika kupikia vyakula mbalimbali, ikiwemo ugali wa unga wa njano. Yeye hakuwa na tatizo la kuweka jina lake. Anaitwa Lawia Makubi mkazi wa Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani. Akandika hivi.

"Kama utakumbuka unga wa njano tuliouita wa Yanga, kabla ya kupika ugali ulikuwa unachekechwa na zile chenga ziliwekwa akiba. Baadaye zinapelekwa tena mashineni kusagwa tena unga ili upikiwe ugali. Mambo yakiwa magumu tena zile chenga kinamama huzipika tena, tuliziita wali wa chenga."

Anachokisema Makubi ni kweli kabisa, miaka ya 1980 wakati wa unga wa Yanga na hata sembe, akinamama walikuwa wanachekecha kwenye chekeche. Unaoanguka chini kwenye ungo ambao ni unga laini ndiyo hupikwa ugali. Unaobaki kwenye chekeche huhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye, kama kupelekwa mashineni ili kupatikana unga mwingine. Na mwingine unaweza kutumika kwa kupikia wali ambao hupikwa kama vile ule wa mchele.

Tena huwa mtamu zaidi mboga yake ikiwa ni maharage. Kinamama wa Pwani chenga hizo huziunga na nazi na wali huo mara nyingi ulitumika asubuhi kunywea chai, na hata wanafunzi wa wakati huo wakitoka shule wanakuta chai na wali wa chenga kwa maharage.

Ni wakati huo ambao hata mashine zenyewe zilikuwa za tabu sana. Ni vijiji vichache sana mikoani vilikuwa na mashine, tena zinazotumia dizeli.

Kwenye miji mikuu kama Dar es Salaam, zilikuwepo za umeme, lakini chache sana, mfano watu wengi Wilaya ya Temeke, walikuwa wanasagia mahindi, au chenga zao maeneo ya karibu na Gerezani, maeneo ya stendi za zamani ya Kamata.

Tukiingia kwa undani sana kuhusu unga wa njano au wa Yanga. Ni unga ulioletwa kutoka nchini Marekani ili kupoza makali ya uhaba wa chakula, uliotokana na uchumi kuyumba, ikiwa ni athari ya Vita ya Kagera. Na baadaye hata mahindi yake nayo yakaletwa, wananchi wakaanza kusaga wenyewe.



Unga wa njano, maarufu kama 'unga wa Yanga' na mahindi yake, yaliyoletwa nchini mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi katikati kupunguza uhaba wa chakula, uliotokana na athari za Vita ya Kagera.



Ugali wa njano, au 'ugali wa Yanga' ambacho kilikuwa ndiyo chakula kikuu kwa Watanzania wengi mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi 1985.

Vita kati ya Tanzania kuanzia Oktoba 30 mwaka 1978 hadi Aprili 11, 1979, kugombea mkoa wa Kagera ambao Rais wa Uganda wakati huo, Idd Amin Dada alidai, mto Kagera na baadhi ya ardhi ya mkoa huo ni mali yake.

Tanzania iliibuka kidedea kwenye vita hiyo kwa kuichakaza Uganda. Hata hivyo vita ni vita. Iliacha makovu pamoja na uchumi kuyumba, kiasi cha Wabongo kutangaziwa 'kufunga mikanda'.

**Mwingine akasema mjomba wake alikuwa anamiliki lingo la miti ambalo pia alikuwa anauza kuni.**

Hali ya chakula ikaanza kuwa mbaya, kiasi cha kupata msaada wa unga na mahindi ya rangi ya njano kutoka nchini Marekani ambao kwa kiasi kikubwa uliwasukuma Watanzania na kutibu njaa, hadi hali iliporejea kwenye hali yake ya kawaida miaka kadhaa baadaye.

Unga huo siyo kama huu ambao tunaouona hivi sasa mweupe. Ulikuwa wa rangi ya njano. Na hata mahindi yake yalikuwa na rangi hiyo. Ukipika ugali unakuwa wa rangi ya njano. Wabongo wakaupachika jina, wakauita 'unga wa Yanga'. Kisa tu kwa sababu ya rangi yake ya njano, ambayo ni moja ya rangi zinazotumiwa na klabu hiyo ya mpira wa miguu Tanzania. Na huu ulikuwa maarufu sana nchini kuanzia mwaka 1980 hadi 1985.

Mbali na uhaba wa chakula. Kulikuwa pia na uhaba wa mahitaji mengine kama sabuni, dawa za meno, miswaki na vitu vingine vingi ambavyo nitakuja kuvielezea siku nyingine kwenye safu hii.

Ukawekwa utaratibu ili wananchi wote wapate, unga huo ukawa haupelekwi kwenye maduka ya kawaida ya watu binafsi. Yakaundwa maduka ya ushirika. Kila wananchi wa eneo fulani walikuwa wakijiorodhesha majina chini ya viongozi wao ambao ni wajumbe wa nyumba kumi na kufungua duka. Haya ndiyo yaliyokuwa yakiitwa maduka ya kaya. Nia ilikuwa nzuri, lakini tatizo utelekezaji wake ukawa mbovu kiasi yakafa kifo cha asili.

Kila mtu anaandikisha kama ana mke na idadi ya watoto alionao. Wenye watoto wengi walipata kilo nyingi za unga kuliko wenye watoto wachache. Na unga, pamoja na bidhaa zingine kama mchele au sukari, mafuta ya taa, siku vikija, vinauzwa kwa kufuata leja iliyopo. Kama ulipata wiki hii, basi mpaka wiki ijayo. Ukimaliza chakula chako mapema utajua mwenyewe.

Wakati huo huo kulikuwa na magari yaliyokuwa yakisambaza chakula, kama unga, mchele, sukari yaliyoitwa Magari ya Ugawaji, siku yakipeleka kwenye maduka binafsi ambapo inakuwa ni kwa nadra sana, foleni yake inakuwa si ya kawaida. Kuna watu wanaweka mawe, makopo kama foleni kuanzia alfariji. Wakati mwingine kunakuwa na ugomvi, patashika nguo kuchanika ili mradi tu kila mmoja anataka yeye awe wa kwanza kupata.

Magari ya Ugawaji yakionekana tu, basi watu wanayafukuza ili kuona wataishia duka gani. Watu waliwahi kufukuza hadi gari la maiti wakidhani ni la ugawaji.

Kutokana na uhaba wa sukari, kulikuwa na sukari guru ambayo wengi waliitumia kama sukari ya kunywea chai.

Kutokana na rangi yake, unaiweka tu kwenye sufuria inaanza kuyeyuka pamoja na maji, basi haina haja tena ya majani ya chai, sukari inakuwa ni hiyo hiyo na majani ni hayo hayo.

Haya ni matukio yaliyotokea huko nyuma hapa nchini ambayo hayatafutika na kubaki kama kumbukumbu kwa vizazi vingi vijavyo kuona Tanzania ilipokuwa wakati mwingine inapitia vipindi vigumu.

**Tuma meseji 0716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

# Korea Kaskazini yadai Covid-19 iliingizwa na vitu vigeni mpakani

**PYONGYUNG,** KOREA KASKAZINI

IMEELEZWA mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19 nchini Korea Kaskazini, ulianza kwa raia wawili kugusa vitu vigeni vilivyoanguka karibu na mpaka wake na Korea Kusini.

Vyombo vya habari vya serikali vya Korea Kaskazini, vilihimiza wananchi kuwa waangalifu kuzunguka vitu ambavyo vinaweza kuwa vimepuliziwa corona kutoka Kusini.

Kwa miaka mingi wanaharakati wa Korea Kusini wana tabia ya kurusha maputo yanayovuka mpaka kwa lengo la kutuma vipeperushi na misaada ya kibinadamu.

Katika kujibu tuhuma hizo, Korea Kusini ilisema hakuna uwezekano Covid kuvuka mpaka kwa njia hiyo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya serikali ya Korea Kaskazini, uchunguzi rasmi uligundua watu wawili ambao waliambukizwa virusi vya Covid 19 mapema katika mlipuko huo baada ya kugusa vitu visivyojulikana karibu na mpaka wa Korea Kusini.


Mwanajeshi mwenye umri wa miaka 18 na mtoto wa miaka 5 walipimwa na kukutwa na virusi hivyo mapema Aprili baada ya kuvipata vitu hivyo kwenye kilima huko Ipho-ri, iliripotiwa.

Tangu wakati huo, vyombo vya habari vya serikali vilisema Virusi vibaya vya Covid-19 vimeenea kwa kasi katika nchini hiyo.

Kutokana na uchunguzi huo, watu wametakiwa kuwa waangalifu na vitu vigeni vinavyokuja na upepo na matukio mengine ya hali ya hewa na maputo katika maeneo ya mpaka.

Yeyote anayegundua kitu kisicho cha kawaida anaagizwa kuripoti mara moja ili kiweze kuondolewa haraka na timu ya dharura ya kupambana na janga la corona.

**BBC**



# Putin awadhihaki viongozi wa Ulaya, wakati akiendelea kuipiga Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

KIONGOZI wa Russia, Vladimir Putin, amewajibu viongozi wa nchi za Magharibi ambao walikejeli picha zake zinazomuonyesha akiwa kifua wazi, akisema itakuwa kitu cha kuchukiza kuwaona wao kuvua nguo zao kama yeye.

Matamshi hayo yametolewa baada ya viongozi wa kundi la G7, kukejeli tabia ya rais huyo kujiweka bila shati katika baadhi ya picha zake.

Putin alitoa wito kwa viongozi wenzake akiwataka kuacha kunywa pombe, badala yake washiriki kwenye michezo.

"Lakini ili kila kitu kiwe sawa, lazima uache kutumia pombe vibaya na maovu mengine, kufanya mazoezi, kucheza michezo."

Pia alikemea maoni ya Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, ambaye alisema kuwa Putin asingeivamia Ukraine kama angekuwa mwanamke.

Wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Putin alisema kuwa tathmini hiyo si sahihi na alitolea mfano Margaret Thatcher ambaye aliamua kuanzisha uhasama katika vita vya Falklands na Malvinas.

Wakati Rais Putin akisema hayo, mashambulizi ya makombora ya Russia yalifanyika kwenye maeneo ya makazi katika mji mmoja karibu na bandari ya Odesa nchini Ukraine.

Mashambulizi hayo yamesababisha vifo vya watu 18 wakiwemo watoto wawili .

Video ya shambulio hilo la alfajiri ya Ijumaa, ilionyesha mabaki ya majengo yaliyoteketea kwa moto katika mji mdogo wa Serhiivka, ulioko kilomita 50 kusini magharibi mwa Odesa.

Taarifa za vyombo vya habari vya Ukraine zimesema makombora yalilenga majengo ya ghorofa katika eneo moja la mapumziko.

Andriy Yermak, mkuu wa ofisi ya rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema kuwa taifa la kigaidi linawauwa watu wao baada kushindwa katika uwanja wa mapigano.

Naibu wa ofisi hiyo ya rais Kirill Tymoshenko, amethibitisha kufariki kwa watu hao 18 na watoto wawili. Katika ujumbe kupitia mtandao wa telegram, msemaji wa serikali katika eneo la Odesa, Serhiy Bartchuk, alisema kuwa watu wengine 30 wamejeruhiwa.



Shambulio hilo linafuatia kuondoka kwa vikosi vya Russia kutoka kisiwa cha Nyoka siku ya Alhamisi, hatua ambayo ilitarajiwa kupunguza tishio katika eneo karibu na Odesa. Kisiwa hicho kiko kando ya njia ya meli yenye shughuli nyingi.

Russia ilichukuwa udhibiti wa kisiwa hicho katika siku za mwanzo za uvamizi nchini Ukraine kwa matarajio ya kukitumia kama eneo la kufanya mashambulizi dhidi ya Odesa.

Rais wa Halmashauri kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, ameliambia bunge la Ukraine kwamba uanachama wa umoja huo unaweza kuafikiwa lakini akalitaka kushinikiza mageuzi ya kupambana na ufisadi. Akiwahutubia wabunge hao kwa njia ya video, Von der Leyen aliwaambia kuwa wameanzisha taasisi za kuridhisha za kupambana na ufisadi lakini zinahitaji kuwa na mamlaka na watu wanaofaa katika nyadhifa kuu.

Hata hivyo, Von der Leyen ililimwagia sifa bunge na serikali ya rais Volodymr Zelensky kwa msukumo wao wa haraka na wenye mafanikio wa kuwa wagombea wa uanachama wa Umoja wa Ulaya.

Alisisitiza kwamba makao makuu ya umoja huo na mataifa wanachama wanaiunga mkono Ukraine katika mapambano yake dhidi ya Russia.

Von der Leyen pia alisisitiza kuhusu haja ya kuendeleza mageuzi ambayo yalianzishwa tangu uasi wa Ukraine wa mwaka 2014 dhidi ya serikali yake ya awali ili kupambana na ufisadi na ubepari katika uchumi wake.

**DW**




Mwanamke akipita karibu na jengo la Imam Al Abbas wakati kimbunga cha mchanga kikipiga mji wa Karbala nchini Iraq juzi. **PICHA: REUTERS**

# Maandamano yaendelea Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

VIKOSI vya usalama nchini Sudan vimefyatua mabomu ya kutoa machozi kuvunja maandamano yaliyodumu kwa siku mbili. Waandamanaji waliingia katika mitaa ya mji Mkuu wa Khartoum, wakipinga mapinduzi ya kijeshi ya mwaka uliopita.

Kulingana na walioshuhudia, walisema waandamanaji walikusanyika tena katika kasri la rais, siku moja tu baada ya karibu watu tisa kuuwawa katika maandamano makubwa ya kulipinga jeshi.

Idadi ya waliofariki kutokana na maandamano nchini humo tangu mapinduzi yalipofanyika imefikia watu 113.

Kifo kimoja zaidi kimeripotiwa jana baada ya mwandamanaji kufariki kutokana na jeraha la risasi alilopata katika maandamano ya Juni 24.

Polisi waliwalaumu waandamanaji hao kwa kuwajeruhi maofisa 96 wa jeshi hilo na wengine 129 waliojeruhiwa pamoja na kuharibu magari na kuwasha moto.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JAMBO FREIGHT LTD,** Inatangaza kupotelewa na Kadi ya pikipiki Aina ya **BAJAJ BOXER** yenye usajili namba **MC 585AAC,** Chassis Namba: **MD2PFPFZZVWA64891** Engine Namba: **PFMBVA02576** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/KIM/RB/235428/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRED ERASTO KINUBI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3674-0069** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. JOSEPH MILLENIUM SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/259233/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEXANDER RECHSTEINER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye namba za usajili **T559 ACY**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa

**ARU/ARU/RB/260953/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSIA SAYI KAPALE** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu mafunzo ya Astashahada index **No SN 2244/0137/2015** Mwaka **2018** Chuo cha St.Gaspar School of Nursing ,kilichotolewa na The National Council for Technical Education **(NACTE)** .Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/256257/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......34 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ABDALLAH SWALEHE MHANDO WA AREA SIX B**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: SWALEHE ABDALLAH MHANDO**

**TANGAZO**

*(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 18 Mwezi 07 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 01 Mwezi 07 Mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**HAKIMU**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Wanakijiji ni kama vile waliachwa njia panda. Wengine waliamini na wengine hawakuamini.

"Yaani kweli yule ni mpenzi wake, wamekaa hapa chini ya paa moja miezi mitatu, halafu kweli aje kumbaka kweli akiwa amejifunika manguo kweli?" Akahoji mama mmoja wakati wakirejea na wenzake mkutanoni.

"Mwenyekiti leo katufunga kamba, mtu atambakaje mpenzi wake?. Halafu kaondoka miezi kibao sasa aje usiku kumbaka? Hivi wale wanavyopendana, hasa Siwatu alivyokuwa anampenda Bakari angekuja tu hivi hivyo angechinjiwa mpaka kuku, leo aje vile, afanye vile, ili iwe nini?" Kijana mmoja akawaambia wenzie, mmoja akajibu.

"Mimi nawaambia wale wameona aibu. wiki ngapi sasa hawajampata aliyefanya kitendo hicho. Kijiji kinapiga kelele, wakaona wakae wamtafute mtu ambaye hayupo wambambikie kesi ili wao wawe salama, waondokane na lawama." Wengi wakakubaliana na hilo.


"Jamani, lakini mimi taarifa za ndani nilipata kusikia, wale hawakuwa wapenzi, walikuwa wanaishi nyumba moja, lakini mmoja analala chini, Siwatu kitandani hadi alipoondoka, na hilo ameshawahi kuniambia mwenyewe Siwatu, inawezekana akapatwa na tamaa, akaja kwa njia ile." Msichana mmoja alitoa siri ambayo haikukubaliwa kwa asilimia tisini. Wengine wakacheka.

"Yaani wale hawakuwa mtu na mpenzi wake kweli? Kawadanganye watoto wadogo. Jinsi walivyokuwa wakiongozana mtaani tu kama kumbikumbi walionyesha kabisa kama ni mtu na mpenzi wake. Mimi nasema hivi, mbakaji hapa hajapatikana, mwenyekiti na kamati yake wametudanganya."

Ilikuwa ni mitazamo ya wanakijiji baada ya mwenyekiti kusema kwamba mbakaji ni Bakari aliyeonekana kuwa ni mpenzi wa Siwatu, kwa kukaa kijijini hapo kwa miezi mitatu, baada ya kuokotwa porini akiwa na majeraha, akinusurika kifo.

Na yeye aliyemuokoa, ndiye aliyembaka.

"Mwenyekiti ana wazimu, yaani Bakari anibake mimi? Hivi anamfahamu au anamsikia? Hakunibaka wakati tunalala wote humu ndani, anibake wakati ameondoka? Kama kijiji kimeshindwa kumpata aliyefanya kitendo hicho kingekaa kimya tu, mimi sina tatizo na mtu kuliko kumsingizia mtu mwingine ambaye kwanza hapa hata hayupo ameshaondoka na sidhani kama atarudi tena." Siwatu alisema akiwa amekaa chini ya mkeka akiwa na Mpaje na Mage ambao walikuja kumtembelea na kumpa yote yaliyojiri kwenye mkutano.




**Hivyo ndivyo baba na mama Sam walivyomfahamu mtoto wao. Baada ya kujidhihirisha kuwa hana tatizo la kiafya, walimuacha tu na tabia yake, ingawa kuna wakati walikuwa wakimuuliza kimtego.**

"Kwani nini shoga yangu, yatafahamika tu, kama ni Bakari kama ni nani yatafahamika tu, hakuna chochote kitakachofichika chini ya jua wifi yangu." Mpaje alimliwaza na kumpa moyo.

*******************************

Anaitwa Samson Dau. Ni kijana aliyezaliwa Kinondoni, Dar es Salaam kwenye familia ya kitajiri. Baba yake alikuwa na mabasi manne ya kusafiria pamoja na malori matano.

Baada ya miaka kadhaa baba yake alifariki dunia na kuwaacha yeye akiwa na dada zake wawili, pamoja na mama yao aliyekuwa tayari mkongwe.

Alisimamia vema mali za baba yake kiasi cha mali hizo kuanza kuongezeka. Sam hakuwa mmoja kati ya wale vijana wa kujikweza kutokana na mali za baba zao, kuzaliwa kwenye familia tajiri. Ndiyo maana pamoja na kuendeleza utajiri wa baba yake aliendelea na maisha yake ya kawaida tu. Ni nadra sana kumuona akiwa disco. Hakuwa anakunywa kilevi chochote kile. Cha ajabu ni kwamba hata hakuwa mpenzi wa wanawake.

Kila mmoja alimshangaa. Hata baba na mama yake walimshangaa. Tangu mdogo mpaka anakua alikuwa hivyo hivyo.

"Hivi huyu mwanao si ameshakuwa mkubwa, mbona hata siku moja sijamuona kwenye harakati za kutafuta wasichana?" Baba yake mzee Dau alimuuliza mama yake.

"Mhh, hata mi sijui mwenzangu, mwanao akitoka shuleni, ndani, ndani na yeye. Akitoka ujue kaenda kuangalia mpira, akirudi ndani." Alijibu mama yake Bi. Tausi.

"Vipi, mzima lakini?"

"Mzima na uzima wake, basi tu mwanao ana tabia ya aibu. Ana aibu huyu mtoto utafikiri mtoto wa kike." Alijibu Bi. Tausi.

Hivyo ndivyo baba na mama Sam walivyomfahamu mtoto wao. Baada ya kujidhihirisha kuwa hana tatizo la kiafya, walimuacha tu na tabia yake, ingawa kuna wakati walikuwa wakimuuliza kimtego.

"Hivi una mpango lini wewe?" Baba yake alimuuliza. Sam anacheka kwa aibu na kuondoa macho kwenye sura ya baba yake.

"Mhh, bado baba?"

"Unasubiri nini wewe wakati umeshamaliza shule, chuo, baba yako uwezo ninao, inakuwaje wewe?"

"Nitaoa baba, ila bado."

"Au huwezi kutafuta nikutafutie. Rafiki yangu Kitau ana binti pale, mrembo kweli na hajaolewa."

"Hapana baba, nitatafuta mwenyewe, nitaoa tu." Alizidi kujibu, lakini kila maswali yanapozidi aibu kwa baba yake inaongezeka.

"Hebu niambie, sasa hivi unae, au huna ndiyo unatafuta?"

"Wala sina, ila nitatafuta."

Wakati mwingine akikaa na mama yake humuuliza.

"Mwenzetu mkwe ni nani sasa?"

"Mkwe gani?"

"Mchumba, nataka nimuone mkwe wangu kabla sijafa."

Ni maneno ambayo huwa yanamfanya Sam kucheka na kumjibu.

"Naogopa kukuletea, usije ukafa bure mama yangu." Akajibu kwa mzaha.

"Yaani we mtoto wewe, hawa dada zako wataolewa, lakini wewe ndiyo mtoto wetu pekee wa kiume, mimi na baba yako tungependa sana kukuona una mtu. Siyo kwamba uoe, hata kumuona tu umekuja naye, umefanya hivi, ili mradi tu mama yako nifurahi na baba yako."

Sam anacheka tena. Mama yake huwa hamuonei aibu kama wengine.

"Kwani wewe mama una wasiwasi gani? Nikimpata nitamleta tu, ila bado sijampata."

"Au una tabia ya kuchaguachagua, shauri yako, kuchagua kwingi..."

Hayo yalikuwa maisha ya Sam na wazazi wake, hadi pale baba yake alipofariki dunia miaka miwili iliyopita.

Tangu baba yake afariki, ameweza kutengeneza faida kubwa kwenye biashara alizoachiwa na baba yake, hivyo utajiri kuongezeka na kuwafanya mama na dada zake kushusha presha kwamba huenda utajiri wao unaweza kuporomoka.

Wakati dada zake ambao ni wadogo zaidi yake walikuwa wameshaolewa, yeye alikuwa bado.

Safari hii hakuna aliyekuwa akimuuliza, si dada zake wala mama yake, walichoangalia wao na kumkubali ni jinsi alivyozibeba biashara za baba yake na kuziendeleza, tena kisomi zaidi kuliko mwanzo.

Akiwa na miaka 27 sasa, akiwa kijana tajiri aliendelea na tabia ile ile ya kutokuwa mlevi, mpenda anasa, badala yake aliendelea kuwa mchapakazi, huruma, upendo, upole na ucheshi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MAKAMBO: LAZIMA TUBEBE FA LEO

**Na Shufaa Lyimo**

HERIETIER Makambo amesema amejipanga vizuri kuhakikisha Yanga inaibuka na ushindi kwenye mchezo wao wa leo wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya timu ya Coastal Union unaopigwa uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makambo amesema mchezo huo utakuwa mgumu na wa ushindani, lakini amejipanga kuiwezesha Yanga kuibuka na ushindi.

"Mchezo utakuwa mgumu kila timu inataka ushindi, nitashirikiana na wachezaji wenzangu tuipe ushindi timu yetu," alisema Makambo.

Makambo alisema mchezo huo hautakuwa rahisi kwani timu ya Coastal Union ina wachezaji wazuri na wenye uzoefu.

"Tunauheahimu mchezo huo kwani tunafahamu mpinzani wetu ana kikosi chenye wachezaji wazuri, hivyo tutaingia tukiwa na tahadhari."

Aliomba mashabiki wao waendelee kuwaombea ili wapate Kombe hilo kwani bila wao hakuna kinachowezekana.

Vile vile aliwataka wajitokeze kwa wingi uwanjani hapo kuwapa sapoti ili wazidi kuwa na morali ya kufanya vizuri.




Waogeleaji wakikata maji katika mashindano tofauti. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Ligi ya Netiboli kuanza Julai 9

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Ligi Daraja la kwanza ya mchezo wa netiboli yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Julai 9 hadi 19 mwaka huu kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa alisema mashindano hayo yatashirikisha timu 29 ambapo timu 23 ni za wanawake na timu 6 ni za wanaume.

"Mashindano hayo yatashirikisha Klabu za Ligi daraja la kwanza mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema lengo la mashindano hayo ni kupata bingwa ambaye atashiriki mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki, mshiriki wa mashindano ya Muungano pamoja na wachezaji watakaoiunda timu ya Taifa.

Alisema kwa upande wa Klabu za mkoa wa Dar es Salaam zinaendelea kujinoa kwa ajili ya kuiweka sawa miili yao.

Alisema Klabu ambazo zitashinda zitapata zawadi ya makombe, ikiwa ni pamoja na fedha ili kuwapa ari wachezaji kujituma zaidi.

Aliwataka watanzania pamoja na wadau mbali mbali wa mchezo huo wajitokeze kwa wingi siku ya mashindano waone vipaji vitakavyooneshwa na wachezaji hao.

## Mashindano ya taifa ya kuogelea kumalizika leo

**Na Mwandishi wetu**

WAOGELEAJI 200 chipukizi kutoka klabu tisa jana walianza kushindania medali na vikombe katika mashindano yanayofanyika kwenye bwawa la kuogelewa la shule ya sekondari ya Shaaban Robert, Dar es Salaam.

Mashindano hayo ya siku mbili yameandaliwa na Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA) chini ya mwenyekiti wa kamati ya maandalizi, Hadija Shebe na yanamalizika leo.

Hadija amezitaja timu ambazo zinazowania taji hilo kuwa ni Bluefins, Champion Rise, FK Blue Marlins, Lake swimming club, MIS Piranhas, Mwanza Swim Club, Pigec, Dar es Salaam Swimming Club na Taliss-IST .

Alisema kuwa timu hizo zimekuwa katika maandalizi makali kwa takribani mwezi mmoja na wanatarajia kuwa na ushindani mkubwa kutoka kila klabu na muogeleaji.

Mashindano hayo yamedhaminiwa na kampuni ya Kilombero Sugar Company Limited ambao ndiyo wadhamini wakuu huku Burger 53, Rap & Roll, Pepsi na F & L Juice ni wadhamini wasaidizi.

Kwa mujibu wa Hadija, mashindano hayo yameshirikisha waogeleaji chipukizi kuanzia miaka 12 kushuka chini na yana lengo la kuibua vipaji vya waogeleaji kwa ajili ya kushiriki mashindano makubwa na ya kimataifa.

## Shamsa atoa neno kwa wasanii

**Na Sabato Kasika**

MSANII nyota wa Bongo Movie, Shamsa Ford, amewataka wasanii wenzake kuishi maisha ya uhalisia kulingana na kipato chao badala ya kutaka sifa kwa watu kwa kujionyesha wana pesa huku wakiumia.

Amesema, baada ya kuuza gari yake kutokana na changamoto za maisha, alikaa miaka miwili bila kuwa na gari, huku akitumia usafiri wa taksi na bajaji na kwamba hakusononeka kwa kuwa maisha ndivyo yalivyokuwa.

"Sikulazimisha kukodi magari kwa ajili ya kujionyesha kwa watu kuwa niko vizuri, nilibeba matatizo yangu na kupambana nayo mwenyewe kwani huo ndiyo ulikuwa uhalisia,"amesema Shamsa.

Katika mtandao wake wa kijamii, ameandika kuwa, kuna wakati alikuwa na mtoto wake kwenye bajaji, huku mtoto huyo akimuuliza kuwa atapata lini gari, na pia akawa anamuomba apige picha akiwa katika magari ya watu wengine.

"Siku nyingine nilimsikia akisali akisema Mungu mpe gari mama yangu, ambapo Mungu amenisaidia nimepata gari ambayo inawezekana isiwe ya thamani, lakini ninaithamini sana," amesema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAPHINHA ATAKIWA
BARCELONA ipo tayari kutoa ofa yenye thamani ya hadi pauni milioni 60 kwa winga wa Leeds, United Raphinha mwenye umri wa miaka 25, katika jitihada za kuwapiku Chelsea kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Mirror)***

### DE LIGT AWANIWA
KLABU ya Chelsea inaendelea na mazungumzo yao ya kutaka kumsajili, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22, lakini Juventus wanataka pauni milioni 102. ***(Telegraph)***

### KIMPEMBE AITAKA CHELSEA
MLINZI wa PSG na Ufaransa, Presnel Kimpembe mwenye umri wa miaka 26, bado anaivutia Chelsea huku timu hiyo ya Ligue 1 ikiwa kwenye soko la kununua beki mpya wa kati. ***(Sun)***

### AKE KUUZWA
KLABU ya Manchester City imesema itamuuza beki wake, Nathan Ake mwenye umri wa miaka 27, iwapo watakuwa na mbadala wake, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi akihusishwa na kurejea katika klabu yake ya zamani ya Chelsea. ***(Manchester Evening News)***

### SPENCE ATAKIWA
KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo ya kutaka kumsajili beki wa kulia wa England, Djed Spence mwenye umri wa miaka 21, kutoka Middlesbrough kwa dau la pauni milioni 15. ***(Sky Sports)***

### FIRMINO AWINDWA JUVE
JUVENTUS inamtaka mshambuliaji wa Liverpool na Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 30, katika mkataba wa kubadilishana na kiungo wao, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27. ***(Calciomercato)***.

### LINGARD NA WEST HAM
KLABU ya West Ham imeongeza juhudi zao za kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### NEVES ABAKI
KLABU ya Wolves imeshinda vita vya kumbakisha kiungo wa kimataifa wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

### PHILLIPS NA CITY
KIUNGO wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, amefanyiwa vipimo vya afya pale Manchester City jana kabla ya kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 45 kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England. ***(Sky Sports)***

### BADIASHILE ATAKIWA
KLABU ya Manchester United imeungana na Newcastle katika vita ya kutaka kumsajili beki wa Ufaransa, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 21 kutoka Monaco. ***(Sky Sport)***

### ROMERO AITAKA MAN
GOLIKIPA wa Argentina, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 35, ana nia ya kurejea Manchester United - mwaka mmoja tu baada ya kuondoka katika klabu hiyo na kuichezea klabu ya Serie A, Venezia. ***(Evening news Manchester)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAHREZ MKATABA MPYA MAN CITY

Mwenyewe ataka kubakia hapo na klabu ipo tayari kumuongezea kama...

**MANCHESTER, England**

RIYAD Mahrez ameiambia Manchester City anataka kubaki na klabu hiyo na yuko tayari kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min.

City walianza mazungumzo na Mahrez kuhusu mkataba mpya mwishoni mwa msimu huu, pamoja na Gabriel Jesus na Raheem Sterling - ambao mikataba yao pia inaisha 2023.

Lakini ingawa Jesus, ambaye hivi karibuni atatambulishwa na Arsenal kwa dau la pauni milioni 45, alikataa masharti mapya na huenda Sterling akaondoka, Mahrez yuko tayari kujitolea kwa mustakabali wake kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Raia huyo wa Algeria alikuwa katika kiwango kizuri msimu wa 2021/22 na alifunga mabao mengi zaidi katika maisha yake ya miaka minne akiwa City.

Alifunga mabao 24 katika michezo 47 katika mashindano yote, na kuyazidi mabao yake ya awali hapo Etihad - mabao 14 msimu wa 2020/21.

Mahrez anaongoza kuwindwa na klabu mbalimbali za Ulaya, huku Real Madrid, Bayern Munich na Paris Saint Germain zikiwa miongoni mwa timu zilizoonyesha nia.

Lakini 90min inaelewa kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ametulia hapo Man City na anataka kuweka mustakabali wake katika timu hiyo inayonolewa na kocha, Pep Guardiola.

Tayari City imewaongeza Erling Haaland na Julian Alvarez kwenye safu yao ya ushambuliaji.

Inaaminika kuwa mazungumzo yanaendelea na City wako tayari kumpa Mahrez mkataba wa miaka mitatu na chaguo la nyongeza ya mwaka mmoja, na wanatumaini kuwa na jambo lililokubaliwa kabla ya kuanza kwa msimu huu.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,010,6
MECHI KALI
LAHTI
VERSUS
INTER TURKU
1 | 3.43
X | 3.48
2 | 1.92
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL KUMREJESHA GNABRY

**LONDON, England**

ARSENAL wanafuatilia kwa karibu mkataba wa Serge Gnabry kule Bayern Munich na wanaweza kujaribu kumrejesha kwenye Uwanja wa Emirates, kwa mujibu wa 90min.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 pale kwenye dimba la Allianz Arena unamalizika msimu wa 2022/23, na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wamedokeza kwamba anaweza kuondoka kwenye dirisha hili.

Kwa mujibu wa 90min Arsenal wanafuatilia kwa uangalifu hali hiyo, huku wakimtaka winga wa Leeds United, Raphinha.

Mkurugenzi wa Bayern, Hasan Salihamidzic wiki iliyopita alifichua kwamba, Gnabry anaweza kuuzwa ikiwa klabu hiyo haiwezi kukubaliana kuhusu masuala ya kuongeza mkataba katika siku za usoni.

"Tunatamani sana kumbakisha. Ninatumaini kwamba, atachagua Bayern. Ikiwa mchezaji hataki kuamua kwa klabu, basi tunaweza kutafuta suluhu ambayo itamfurahisha kila mtu," alisema akinukuliwa na Sky Sport.

Gnabry alijiunga na Washikabunduki akiwa na umri wa miaka 16 na alicheza 18 chini ya kocha Arsenal Wenger, ingawa alitumia mwaka wake wa mwisho nchini England kwa mkopo katika klabu ya West Bromwich Albion iliyokuwa inanolewa na kocha, Tony Pulis.

Alijiunga na Werder Bremen kwa pauni milioni 5 mwaka wa 2016 na akasaini Bayern Munich muda mfupi baadaye, akitumia msimu wa 2017/18 huko Hoffenheim kabla ya kujiunga na timu ya kwanza kule Bavaria.



# Richarlison atua rasmi Tottenham

**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham Hotspur imemsajili mshambuliaji wa Brazil, Richarlison kutoka Everton kwa mkataba wa miaka mitano unaoaminika kuwa wa thamani ya pauni milioni 60.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alifunga mabao 10 na kutoa pasi tano za mabao huku akiisaidia Everton kuepuka kushuka daraja msimu uliopita.

Alifunga mabao 43 katika mechi 135 za ligi Kuu akiwa na Toffees hao baada ya kujiunga kutoka Watford Julai 2018.

Walimsajili Richarlison kwa pauni milioni 11.5 kutoka Fluminense ya Brazil mwaka 2017.

Akicheza kama mshambuliaji wa kati, Richarlison alimaliza kama mfungaji bora Everton katika michuano yote katika misimu yake miwili.

Alianza mechi yake ya kwanza ya kimataifa akiwa na Brazil Septemba 2018 akiingia kipindi cha pili katika ushindi wao wa 2-0 dhidi ya Marekani na amefanikiwa kucheza mechi 36, akifunga mabao 14.

Mwaka 2019, alijumuishwa katika kikosi cha wachezaji 23 kwenye michuano ya Copa America na akafunga katika fainali huku Brazil ikitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza tangu 2007.

Alicheza pia katika michezo ya Olimpiki ya majira ya joto ya mwaka 2020 kule Tokyo, akimaliza kama mfungaji bora wa mashindano hayo akiwa na mabao matano huku timu yake ikishinda dhahabu.

Tottenham wamemleta fowadi huyo huku wakijiandaa kwa msimu ambao wamefuzu kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya.

Tayari wamemsajili mlinda mlango wa England, Fraser Forster kwa uhamisho huru baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kuondoka Southampton, pamoja na winga wa Croatia, Ivan Perisic kwa uhamisho wa bure kutoka Inter Milan na mlinzi wa Brighton na Mali, Yves Bissouma.

89,585/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.7.2022 | 22:00 | Ituano SP vs Criciuma SC | 2.41 | 2.93 | 3.18 |
| 2.7.2022 | 22:30 | Fluminense vs Corinthians | 2.23 | 3.04 | 3.48 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Santos vs Flamengo | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Ceara CE vs Internacional | 2.49 | 3.04 | 2.99 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Toronto vs Seattle Sounders | 2.65 | 3.75 | 2.43 |
| 3.7.2022 | 02:30 | CRB AL vs Guarani SP | 2.39 | 2.82 | 3.37 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Gimnasia y Esgrima vs Defensa Justicia | 2.27 | 3.39 | 3.19 |
| 3.7.2022 | 13:30 | Suwon Samsung vs Incheon Utd | 2.49 | 3.19 | 2.89 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Varbergs Bois vs IFK Varnamo | 2.49 | 3.15 | 2.90 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Djurgardens IF vs Hammarby | 2.23 | 3.42 | 3.08 |
| 3.7.2022 | 18:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.52 | 3.16 | 2.81 |
| 3.7.2022 | 18:30 | BK Hacken vs Elfsborg | 2.41 | 3.52 | 2.73 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Union Santa Fe vs Lanus | 2.25 | 3.20 | 3.30 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Aalesunds vs Stromsgodset | 2.24 | 3.47 | 3.02 |
| 3.7.2022 | 21:00 | Barracas Central vs San Lorenzo | 2.90 | 3.15 | 2.50 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.99 | 3.04 | 2.48 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Bahia BA vs Gremio | 2.63 | 2.78 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 02/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1999 | Igilik vs FC Zhetysu | 6.30 | 4.33 | 1.41 |
| 14:00 | 3187 | Okzhetpes vs Kyran Shymkent | 1.77 | 3.49 | 4.03 |
| 14:00 | 3762 | Seongnam Ilhwa vs Gangwon | 3.05 | 3.15 | 2.20 |
| 14:00 | 4409 | Toten vs Floro | 8.47 | 6.11 | 1.22 |
| 14:00 | 4522 | Brann 2 vs Sola | 1.36 | 5.60 | 6.20 |
| 14:00 | 4951 | Fyllingsdalen vs Ready | 1.60 | 4.32 | 4.12 |
| 14:30 | 2874 | Shandong Luneng vs Guangzhou RF | 1.05 | 8.65 | 29.50 |
| 15:00 | 1315 | Flekkeroy vs Arendal | 3.13 | 3.77 | 1.94 |
| 15:00 | 2429 | Stord vs Fana | 3.24 | 4.51 | 1.76 |
| 15:00 | 2796 | Grorud IL 2 vs Os TF | 2.39 | 3.69 | 2.44 |
| 15:00 | 3450 | Skiljebo SK vs Orebro Syrianska | 2.46 | 3.80 | 2.44 |
| 15:00 | 3998 | Skeid Fotball 2 vs Sandviken | 1.58 | 4.90 | 3.82 |
| 15:00 | 4017 | Shakhter Karagandy vs Aktobe | 2.22 | 3.00 | 3.15 |
| 15:00 | 4149 | Vmfd Zalgiris-3 vs FK Ekranas | 2.06 | 3.65 | 3.15 |
| 15:00 | 4165 | IK Gauthiod vs Grebbestads IF | 1.32 | 5.09 | 6.85 |
| 15:00 | 4454 | Honka vs IFK Mariehamn | 1.43 | 4.22 | 6.08 |
| 15:00 | 4832 | Narpes Kraft vs Vifk Vaasa | 2.22 | 4.01 | 2.50 |
| 15:00 | 4891 | Oppsal IF vs Nordstrand | 4.62 | 4.32 | 1.53 |
| 16:00 | 1386 | Dalkurd FF vs Landskrona Bois | 2.24 | 3.51 | 3.05 |
| 16:00 | 1505 | Lyn Oslo vs Lokomotiv Oslo FK | 1.22 | 6.10 | 8.65 |
| 16:00 | 1771 | Akra vs Bjarg | 3.74 | 4.03 | 1.71 |
| 16:00 | 3201 | Ostersunds vs Utsiktens BK | 3.21 | 3.52 | 2.15 |
| 16:00 | 3938 | Melaka vs Johor Darul Takzim | 6.88 | 4.72 | 1.35 |
| 16:00 | 4644 | AIK Football vs Mjallby | 1.41 | 4.03 | 7.08 |
| 16:00 | 4969 | Albion FC vs Torque | 4.02 | 3.58 | 1.75 |
| 17:00 | 1235 | HJS Akatemia vs Salpa Salo | 2.65 | 3.64 | 2.23 |
| 17:00 | 1692 | Trans Narva vs Paide Linnameeskond | 7.06 | 4.80 | 1.33 |
| 17:00 | 2192 | Atyrau vs Taraz | 2.38 | 2.95 | 2.95 |
| 17:00 | 3285 | AC Oulu vs VPS Vaasa | 3.00 | 3.25 | 2.18 |
| 17:00 | 3479 | Kerho 07 vs FF Jaro | 2.75 | 3.48 | 2.23 |
| 17:00 | 3875 | HJK Helsinki vs KuPS Kuopio | 2.07 | 3.19 | 3.29 |
| 17:00 | 4433 | Jerv vs Haugesund | 3.06 | 3.46 | 2.18 |
| 17:00 | 4483 | Kaisar Kyzylorda vs FK Ekibastuz | 1.39 | 4.41 | 6.47 |
| 17:00 | 5049 | Pepo Lappeenranta vs EIF Ekenas | 3.33 | 3.67 | 1.90 |
| 18:00 | 1558 | Lahti vs Inter Turku | 3.43 | 3.48 | 1.92 |
| 18:00 | 4554 | Osters IF vs Skovde Aik | 1.52 | 4.17 | 6.10 |
| 18:30 | 1191 | Helsingborg vs Kalmar | 3.54 | 3.19 | 1.98 |
| 19:00 | 2059 | Dinamo Minsk vs Isloch | 1.55 | 3.76 | 5.27 |
| 19:00 | 4477 | Odd Ballklubb vs Bodo Glimt | 4.22 | 3.92 | 1.72 |
| 19:00 | 5029 | Vestmannaeyjar vs Breidablik | 5.09 | 4.41 | 1.48 |
| 19:30 | 2875 | Tallinna JK Legion vs Flora Tallinn | 20.53 | 7.24 | 1.10 |
| 20:00 | 1058 | Parnu JK Vaprus vs Tammeka Tartu | 3.94 | 3.84 | 1.71 |
| 20:00 | 5071 | Vilniaus Riteriai vs Zalgiris Kaunas | 2.16 | 3.04 | 3.24 |
| 21:30 | 5297 | CA Tigre vs Talleres | 1.77 | 3.28 | 4.31 |
| 21:45 | 1946 | Sligo Rovers vs Shelbourne | 2.14 | 3.00 | 3.34 |
| 22:00 | 4690 | CD Palestino vs Union Espanola | 2.30 | 3.24 | 2.80 |
| 22:30 | 3570 | Juventude RS vs Atletico Mineiro | 4.22 | 3.24 | 1.81 |
| 22:30 | 4126 | Fluminense vs Corinthians | 1.86 | 3.06 | 4.24 |
| 23:00 | 3848 | Imbabura Sporting Club vs Guayaquil City | 3.29 | 3.29 | 2.03 |
| 23:15 | 3855 | Club Cienciano vs Univ San Martin | 1.23 | 5.70 | 9.04 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM YAANZA KUSHUSHA VIFAA

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache tu baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, klabu ya Azam imeonekana haitaki mchezo kwani imeamua kujiandaa na michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika na maandalizi ya msimu ujao kwa kusajili wachezaji wawili kutoka nchini Ivory Coast.

Klabu hiyo juzi jioni iliwatambulisha wachezaji Kipre Junior ambaye ni mshambuliaji na kiungo mshambuliaji Tape Edinho, kila mmoja akisajiliwa kwa mkataba wa miaka mitatu.

Taarifa zinasema kuwa mmiliki wa klabu hiyo, Yusuph Bakharesa ameamua kuingia mwenyewe mstari wa mbele kwenye usajili, kuhakikisha timu hiyo inarejesha makali na heshima yake kama miaka ya nyuma.

"Mashabiki zangu na mashabiki wa Azam FC, nimeamua, sasa mtafurahi sana." Ni kauli ya mmiliki huyo aliyoitoa wakati wa utambulisho wa wachezaji wao.

Klabu hiyo imewatambulisha rasmi wachezaji hao na kuandika kwenye mtandao wao rasmi wa instagram.

"Tunayo furaha kuwataarifu kuwa tumeingia mkataba wa miaka mitatu na kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Ivory Coast, Kipre Junior."

Nyota huyo aliyekuwemo kwenye kikosi bora cha msimu huu wa Ligi Kuu ya Ivory Coast, amewahi kusajiliwa na miamba ya Ufaransa, Strarsbourg msimu wa 2017/2018. Aliwahi kuwatumikia vigogo wa Ivory Coast, Asec Mimosas, 2018-2020.

"Tunayo furaha kuwataarifu kuwa tumeinasa saini ya kiungo mshambuliaji kutoka Ivory Coast, Tape Edinho, kwa mkataba wa miaka mitatu.

"Edinho tumemnunua kutoka timu ya ES Bafing ya kwao, ambapo mkataba huo utamfanya kuhudumu ndani ya viunga vya Azam Complex hadi mwaka 2025."

Nyota huyo mwenye uwezo mkubwa, amesaini mkataba huo mbele ya mmiliki wa timu hii, Yusuf Bakhresa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Mkali huyo amechaguliwa kwenye kikosi bora cha Ligi Kuu ya Ivory Coast msimu huu kutokana na ubora wake wa kuhenyesha wachezaji wa timu pinzani.

Msimu uliomalizika, amefanikiwa kufunga jumla ya mabao matano na kuchangia pasi tisa zilizozaa mabao." ilimaliza taarifa hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salim Kali (Mwenye jezi ya Tanzania) akiongoza mamia ya wakazi na viongozi katika mbio za kuuzunguka mji huo kwa lengo la kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika zoezi la sensa ya watu na makazi litakalofanyika Agosti 23 mwaka huu. **PICHA:VITUS AUDAX**

# Mpole: Thamani yangu imeongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

MFUNGAJI bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara, msimu wa 2021/22, George Mpole amesema tuzo hiyo itamuongezea heshima na kumpa thamani kubwa katika dirisha la usajili lililofunguliwa jana.

Mshambuliaji huyo wa Geita Gold amesema haikuwa rahisi kwake kufikia mafanikio hayo na ilimbidi kujitoa ili kuweka rekodi hiyo.

"Bado sijajua msimu ujao nitacheza wapi lakini tuzo hii ya ufungaji bora imeongeza thamani yangu kuelekea dirisha kubwa la usajili, sababu huu ni muda wa kuvuna kile nilichopanda," amesema Mpole.

Mshambuliaji huyo aliyefunga mabao 17, amewashukuru wachezaji wenzake na benchi la ufundi chini ya Kocha Fred Minziro kwa kumwamini na kumpa nafasi.

Mpole pia amempongeza mpinzani wake Fiston Mayele wa Yanga kwa ushindani aliomwonesha kipindi chote.

Klabu za Azam, Simba na Yanga zinatajwa kumwania mshambuliaji huyo kutokana na uwezo aliouonesha msimu huu katika umaliziaji.

Rekodi hiyo ya Mpole inamfanya kuwa mshambuliaji wa pili mzawa kuibuka kinara wa mabao katika misimu ya hivi karibuni ambapo msimu uliopita alikuwa John Bocco aliyefunga mabao 16.

Dirisha la usajili kwa klabu za Ligi Kuu, Championship, daraja la kwanza na Ligi Kuu ya Wanawake msimu wa 2022/2023 limefunguliwa jana na litafungwa Agosti 31, 2022.

# Michezo

UKURASA 21
Jumamosi Julai 2, 2022
Nipashe



**Mahrez mkataba mpya Man City**



Wachezaji na viongozi wa timu ya Yanga wakiwa na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mohamed mara baada ya kutoa msaada kwenye kituo cha kupambana na matumizi ya dawa za kulevya cha Njiro Recovery Sober House, jana. **PICHA: YANGA**

# YANGA, COASTAL KAZI MOJA TU LEO

## ●●●Ni katika fainali ya kombe la Shirikisho, kila moja yapania kulibeba taji hilo kwa sababu...

**Na Adam Fungamwango**

LEO kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Mabingwa wa Soka Tanzania Bara, Yanga huenda ikaweka rekodi iliyowekwa na watani zao Simba iwapo itapata ushindi na kutwaa Kombe la Shirikisho la soka Tanzania, TFF, FA, dhidi ya Coastal Union.

Yanga imepania kuchukua kombe hilo na kuweka rekodi iliyowekwa na Simba misimu miwili iliyopita ilipokuwa ikitwaa Ubingwa wa Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA.

Tayari Yanga imeshatawazwa kuwa mabingwa wapya, hivyo kilichobaki ni kuchukua kombe hilo ili kuwa kama Simba ilivyofanya msimu uliopita.

Yanga ilifungwa fainali msimu uliopita na Simba bao 1-0 kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, mechi ikichezwa Julai 25 mwaka jana, pia Wekundu wa Msimbazi walichukua msimu mmoja kabla ya huo kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mjini Sumbawanga walipoitwanga Namungo mabao 2-1, Agosti 2, 2020.

Kocha msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amewataka wachezaji wake kusahau kila kitu kilichopita, badala yake akili na nguvu zote wazielekeze kwenye mchezo huo muhimu.

"Kikosi kiko vizuri, hatuna majeruhi, badala yake ni yule yule Yacouba Songne ambaye ni majeruhi wa muda mrefu. Tunakwenda fainali muhimu kwetu, wanachama na mashabiki wetu. Wachezaji na kila mtu anapaswa kusahau yaliyotokea kwenye ligi na sherehe, tujiandae na mechi hiyo," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu, Juma Mgunda amesema kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa na sasa wanaisubiri mechi hiyo.

"Vijana wako vizuri, tuko tayari kucheza na Yanga. Tumejipanga na tumekuja kushindana. Tunajua huu ni mchezo wa fainali ambao hauhitaji pointi wala sare, zaidi ya matokeo ya ushindi tu, yanatakiwa matokeo mazuri tu. Hatuna majeruhi, tunajua Yanga ni timu nzuri, ndiyo mabingwa na tunawaheshimu, lakini na sisi tumejipanga na nimewaambia wachezaji wangu wakatekeleze yale niliyowaambia, wakitekeleza wajibu wao vema, nina uhakika tutapata ushindi," alisema Mgunda.

Mara ya mwisho Yanga kutwaa Kombe la FA ilikuwa ni msimu wa 2015/16 ilipoichapa Azam FC mabao 3-1 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Mei 26, 2016 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, yakifungwa na Amissi Tambwe alipachika mawili na Deus Kaseke, bao ya kufutia machozi la Azam likifungwa na Didier Kavumbagu.

# Simba SC yamshangaa Morrison

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imedai kushangazwa na Benard Morrison kutoa shutuma kwa viongozi kupitia vyombo vya habari badala ya kufuata taratibu zinazohusika kama anaona hakutendewa haki.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu amesema kuwa anamshangaa mchezaji huyo kudai alilazimishwa kwenda mapumziko ya lazima wakati hakuwa na matatizo ya kifamilia, lakini alishindwa kulalamika au kukataa wakati huo hadi kuibuka sasa, hivyo kuonesha huenda analishwa maneno.

Murtaza alisema hayo juzi, ikiwa ni siku moja baada ya mchezaji huyo ambaye anamaliza mkataba wake na klabu hiyo Agosti 14, kutoa maelezo kadhaa, ikiwemo shutuma kwa baadhi ya viongozi, akidai hata alipoandikiwa barua ikidai kuwa alikuwa na matatizo ya kifamilia, hivyo aende kwao akayatatue, haikuwa kweli kwamba alikuwa na matatizo.

Alisema hayo alipokuwa akihojiwa na chombo kimoja cha habari.

"Alisaini mkataba wa ajira na Simba kwa ridhaa yake, kama alikuwa hajaridhishwa na kitu chochote mbona hakusema au kufuata taratibu zilizopo kwa sababu kwenye mkataba kumeainishwa haki zake na za klabu, kwa nini hakufanya hivyo? Yeye ndiye aliyetaka ruhusa kwenda kutatua matatizo ya kifamilia, klabu ikampa, akakubali kwa nini leo amegeuka ghafla baada ya kurejea kutoka huko alikotoka? Na kama alikuwa hana la kufanya huko kwa nini alikwenda kwao?." Alihoji Mangungu.

Alisema Morrison bado ni mchezaji wa Simba na kuachwa au kubaki itategemea benchi la ufundi litakavyoamua.

Kuhusu kukataliwa barua ya kuondoka kwenye klabu hiyo, mwenyekiti huo alisema wapo wachezaji ambao wao na klabu zinazowataka zimeomba na wamepata, ila yeye ameamua kuomba kwa kupitia mitandao ya kijamii, kitu ambacho si utaratibu.

"Yeye ameamua kujadiliana kwenye vyombo vya habari badala ya kuiambia klabu inayomtaka kuomba barua rasmi, anaomba kupitia mitandao ya kijamii, basi aendelee," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >